# Nipashe

Alhamisi Februari 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579847

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Baba amtorosha mtoto mkobani toka hospitalini

UKURASA 25




UKURASA 13

MAUZO YA KOROSHO:

# Serikali yawaita wanunuzi binafsi

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### IGP SIRRO ATANGAZA OPERESHENI KUSAKA WAGANGA WA JADI

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, ametangaza operesheni kuwasaka waganga...

## Matibabu ya Ruge yafikia mil.650/-



UKURASA 3



UKURASA 2

Rais John Magufuli, akiagana na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation kwa Afrika na Mashariki ya Kati, Willem Jacobs, baada ya mazungumzo na ujumbe wake, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mabilioni ya Barrick Machi

MICHEZO YANGA YAANGUSHA MNINGA WA KIRUMBA UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Majaliwa awatega DC, DED kwa JPM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo, Sada Malunde na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Wende Ng'ahara, wamalize tofauti zao na wasipojirekebisha atamshauri Rais John Magufuli kufanya maamuzi mengine. Alisema kitendo cha viongozi hao kutoelewana kinaonyesha mfano mbaya kwa watumishi walio chini yao, hivyo amewataka wajirekebishe mara moja kwa kuwa wameaminiwa na serikali kuliongoza eneo hilo na si kuwachanganya wananchi.

Waziri Mkuu alitoa karipio hilo jana, wakati akihutubia wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa mpira wa Shule ya Msingi Nyakanazi, Kijiji cha Nyakanazi, Biharamuko mkoani Kagera.

Alisema kutokuelewana kwa viongozi hao ambao wakati mwingine wanatuhumiana kufanyiana vitendo vya kishirikina kumesababisha kuzorota kwa shughuli za maendeleo katika wilaya. "Mliletwa hapa kuiwakilisha serikali na kusimamia maendeleo ya wananchi nyie mnagombana."

Awali, Waziri Mkuu akiwa njiani kuelekea mkoani Kagera alitembelea kambi ya Nyanza Roads inayojenga barabara ya Nyakanazi-Kabingo, inayounganisha mikoa ya Kigoma na Kagera na kusema kuwa hajaridhishwa na kasi ya mkandarasi huyo.

Barabara hiyo inayojengwa kwa kiwango cha lami inaurefu wa kilomita 50 na ilianza kujengwa 2014, ilitarajiwa kukamilika 2016, ambapo kwa sasa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 60.

"Sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara hii, mkandarasi na mhandisi mshauri wote wanaonekana hawapo makini katika kufanya kazi hii. Hii ni aibu kwa makandarasi wa ndani ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia kutokupewa kazi kumbe hawako makini."

# Serikali yaita wanunuzi binafsi korosho

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeruhusu kampuni na watu binafsi kununua kiasi chochote cha korosho msimu ujao na wanaotaka kufanya hivyo wameagizwa kuwasilishwa maombi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, alisema mpaka sasa serikali imeshakusanya tani 221,060 zenye thamani ya Sh. bilioni 718, ambazo zimehifadhiwa kwenye maghala.

Alisema kikubwa wanachotakiwa kuzingatia wanunuzi wote ni kutambua serikali imenunua korosho hizo kwa bei ya Sh. 3,300 kwa kilo na gharama za usafirishaji na zinginezo.

Kakunda alisema serikali imeweka kipaumbele cha kutosha kwa viwanda vya ndani ya nchi ili kuimarisha uwezo wa ndani wa kubangua korosho na kujenga mnyororo wa thamani kwa zao hilo na kuongeza ajira na uwekezaji kwenye viwanda.

Pia alisema serikali iko mbioni kutia saini mkataba wa kuuza tani 15,000 za korosho kwa Kampuni ya Bi-Southern ya nchini.

"Licha ya kampuni ya Indo Power Solution ya Kenya kununua tani 100,000 za korosho, pia kampuni ya Bi-Southern ya hapa nchini iko kwenye mchakato wa mwisho wa kununua korosho ghafi tani 15,000 na hivi sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapitia mkataba wa ununuzi wa korosho hizo," alisema.

Kuhusu kampuni na watu binafsi, Waziri Kakunda, alisema baada ya serikali kujiridhisha kwamba

INAENDELEA UK. 8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu Kinampanda, Maulid Njau (kulia), juu ya maboresho na ukarabati wa chuo hicho, wilayani Iramba Mkoa wa Singida jana. **PICHA: OMR**


Gili High School

**GILI SEKONDARI**

**NAFASI ZA KIDATO CHA TANO (FORM FIVE).**

**SHULE NZURI YA BWENI YA WASICHANA-KIBAHA**

Gili Secondary inatangaza nafasi za kidato cha tano " A level" tahasusi zifuatazo: PCB, PCM, CBG, HGK, HGL, HKL, HGE, ECA

Gili ni shule ya wasichana ya bweni tu, imesajiliwa na wizara ya elimu kwa namba S.4375 na baraza la mitihani la taifa kwa namba S.4565. Shule ipo Kibaha maili moja B, kilometa mbili kutoka barabara ya morogoro.

***Kwa matokeo na taarifa nyinginezo tembelea tovuti yetu***

**www.gilisecondary.ac.tz**

115073002

**PRE FORM V ITAANZA TAREHE 23/03/2019 NA PRE FORM ONE ITAANZA MWEZI WA TISA MWAKA HUU**

**JINSI YA KUJIUNGA**

Fomu zinatolewa shuleni na Msimbazi Centre chumba namba 9 au kwenye tovuti yetu www.gilisecondary.ac.tz . **SIMU:** 0714 477 216, 0622 564 660, 0753 963 866, 0692 796 969

**Email:** gilihighschool@gmail.com **Facebook:** Gili High School **Instagram**: Gili High School, **Twitter:** gilihighschool

**KARIBU.**


# Mabilioni ya Barrick kutua Machi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold anayeshughulikia Afrika na Mashariki ya Kati, Dk. Willem Jacobs, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema katika mazungumzo hayo, Dk. Jacobs alimhakikishia Rais kuwa watalipa fedha walizoahidi mwezi ujao.

Baada ya mazungumzo hayo, kwa mujibu wa taarifa hiyo, Dk. Jacobs aliyeongozana na washauri wa Barrick Gold Corporation, Rich Haddock, Duncan Bullivant na Wicus du Preez, alisema wamekutana na Rais Magufuli ili kumhakikishia kuwa makubaliano yaliyofikiwa Oktoba 19, 2017 watayatekeleza kikamilifu baada ya kampuni kubwa ya uchimbaji dhahabu ya Rand Gold ya Afrika Kusini kuungana na Barrick Gold Corporation katika umiliki, uwekezaji na menejimenti.

Dk. Jacobs alisema hakuna

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/02/2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Mtwara** kuelekea **Mbeya,** magari hayo yana namba za usajili:

**T221BYM/T887DJB**
**T636DFA/T837DJB**
**T133CCP/T574BZB**
**T296CZS/T900BAZ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 27.0
Upana - mita 5.50
Kimo - mita 6.40

3. Njia itakayotumika: **Mtwara hadi Mbeya** Kupitia **Makambako,**
Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 06:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215065902

HABARI KITAIFA

# Matibabu ya Ruge mil. 650/-, aomba msaada

**Na Romana Mallya**

GHARAMA za matibabu ya Mkurugenzi wa vipindi vya Clouds Media, Ruge Mutahaba, ambaye yuko Afrika Kusini akiendelea kutibiwa tatizo la figo, gharama sasa zimefikia zaidi ya Sh. milioni 650.

Kutokana na hali hiyo, mdogo wa Ruge, Mbaki Mutahaba, akihojiwa kwenye kipindi cha 360 cha Clouds TV, alisema Ruge alianza kuumwa mwaka jana.

"Gharama za matibabu Afrika Kusini ni kubwa kwa siku inaweza kufikia milioni tano hadi sita, tunaomba kwa ambao watatamani kumsaidia watume chochote kupitia akaunti namba mdogo wa Ruge, Kemilembe Mutahaba, 0752 222 210," alisema.

Alisema watu wanaweza kutuma ujumbe mfupi wa pole, faraja au kutuma chochote kwa ajili ya kusaidia matibabu yake. Kuhusu historia ya kuumwa kwake, Mbaki alisema Ruge alianza kuumwa mwaka jana na kabla ya kupelekwa Afrika Kusini alilazwa Hospitali ya Kairuki na baadaye India.

"Jopo la madaktari na Kairuki na Muhimbili wakasema apelekwe Afrika Kusini kwa sababu ni karibu ila matibabu ya huko yana gharama kubwa," alisema na kuongeza:

"Ila msaada ni kubwa ukianza na mheshimiwa Rais John Magufuli, alishatoa msaada mkubwa sana na amekuwa akipiga simu kujua hali yake kila wakati ila kule gharama ya matibabu ni kubwa kwa siku inaweza kufika milioni tano mpaka sita," alisema.

Mbaki alisema mwezi Aprili alianza kuumwa bila kujua ni tatizo la figo na mwezi uliofuata ndipo alipopata majibu ya hospitali kuwa anasumbuliwa na figo.

Alisema baada ya kufika India, walimwambia figo zake hazina ulazima wa kubadilishwa.

"India hakukaa muda mrefu alirejea Tanzania na kuendelea na matibabu, lakini baadaye hali ikabadilika mara ya pili akalazwa Kairuki, kutokana na hali yake iliyokuwa ilipofika mwezi Septemba mwaka jana madaktari wakapendekeza apelekwe Afrika Kusini," alisema.

Alisema baada ya kufika Afrika Kusini mambo mengine yakaibuka yanayohusiana na figo, hivyo madaktari wakawa wanatibu na mengine zaidi ya figo.

"Kinachotia moyo yale yaliyokuwa yanasababishwa na figo yametulia, changamoto ni kumrudisha kwenye hali yake ya kawaida kwa sababu amekaa hospitali muda mrefu, hivyo kwa sasa amekuwa mgonjwa wa kumsaidia kupata nafuu, hali yake siyo mbaya inaridhisha ikilinganishwa na awali," alisema.

Alisema anaamini wakiendelea na maombi Ruge ambaye amesaidia sana kuibua vipaji wa wasanii wengi wa kizazi kipya, atavuka hilo alilonalo sasa.

## IGP atangaza operesheni kusaka waganga jadi

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, amesema mikoa yote nchini imeanza operesheni kali dhidi ya waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi kwa sababu wamekuwa chanzo cha mauaji ya watu nchini.

IGP Sirro alitoa msimamo huo jana katika kijiji cha Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo pamoja na viongozi wengine wa Wilaya ya Kahama.

Alisema Jeshi la Polisi halina ugomvi na waganga wa jadi, bali linawatafuta wale wanaojihusisha na kupiga ramli chonganishi wanaohusishwa na vitendo vya mauaji.

Alisema hali ya ulinzi na usalama nchini ni shwari kwa kuwa tayari wamefanikiwa kuanza kudhibiti mauaji ya watoto katika mikoa ya Njombe na Simiyu.

Sirro aliseka Jeshi la Polisi lilifanikiwa kudhibiti na kukomesha mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino, lakini kwa sasa yameanza kujitokeza mauaji ya watoto ambayo yanatokana na uchonganishi wa waganga wa jadi. IGP alisema ni lazima wawasake na kuwachukulia hatua kali na kwamba suala la kupiga ramli chonganishi ni ushamba ambao umepitwa na wakati.

Akitoa taarifa ya ulinzi na usalama ya Halmashauri ya Ushetu, Mkuu wa Polisi Ushetu, Tabita Makaranga, alisema halmashauri hiyo inakabiliwa na changamoto ya matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, wivu wa mapenzi na migogoro ya kurithi mali.



## Muuza duka auawa na 'Panya Road'

**Na Romana Mallya**

MUUZA duka, mkazi wa Ukonga Mazizini, jijini Dar es Salaam, ambaye jina lake halijafahamika, ameuawa kwa kuchomwa kisu na kundi la vijana wanaodaiwa ni 'panya road'.

Inadaiwa kuwa kundi la vijana hao lilifika dukani kwake na kumwamrisha atoe fedha zote za mauzo.

Kaimu Kamanda wa Mkoa wa Polisi wa Ilala, Ernest Matiku, aliliambia Nipashe juzi kuwa tukio hilo lilitokea Jumatatu saa 1:00 usiku.

Alisema wakati wa tukio hilo, vijana hao walikuwa wakitoka kwenye mpira Majohe na baada ya kufika eneo hilo la Mazizini walikwenda moja kwa moja kwenye duka hilo na kuanza kufanya vurugu, huku wakimshinikiza muuza duka awape fedha.

"Walianza kufanya vurugu na kumwamrisha atoe fedha, alipokataa waliingia dukani na mmoja wao alikuwa na kisu alikitoa na kumchoma nacho kijana huyu aliyekuwa anauza duka na wao kuondoka," alisema.

Alisema mtu huyo alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ilala ya Amana lakini baadaye alifariki dunia.

Kamanda Matiku alisema hadi sasa wanawashikilia vijana sita katika Kituo cha Polisi Stakishari na kwamba juhudi za kuwasaka wengine zinaendelea.



Wananchi wakipita jirani ya rundo la takataka lililotelekezwa kwa muda mrefu bila ya kuzolewa katika soko la Temeke Stereo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni changamoto kubwa katika masoko mengi katika jiji hilo na kusababisha kero kwa wafanyabiashara na wateja wao. **PICHA: SALOME KITOMARI**

# Maalim Seif ateua wajumbe 9 wa bodi

**Na Enock Charles**

SIKU moja baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kutengua uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF), walioteuliwa na Mwenyekiti wa Chama hicho anayetambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Prof. Ibrahim Lipumba, chama hicho upande wa Katibu Mkuu, Maalim Seif Shariff Hamad, umeteua wajumbe wapya wa bodi hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na Naibu Mkurugenzi wa Habari wa chama hicho upande wa Maalim Seif, Mbarala Maharagande, iliwataja wajumbe hao wapya kuwa ni Abdallah Said Khatau, Ali Mbaraka Suleiman, Yohana Mbelwa, Mohammed Nassoro Mohammed, Dk. Juma Amei Muchi, Zumba Shomari Kipanduka, Mwanawetu Said Zarafi, Mwana Masoud Ali na Blandina Obas Mwasabwite.

Uamuzi uliotolewa juzi na Jaji Benhajj Masoud ulibatilisha uteuzi wa wajumbe wa bodi hiyo, kwa hoja kwamba uteuzi wao haukuzingatia Sheria ya Muungano wa wadhamini ambao ndiyo unasimamia usajili wa wajumbe wa bodi za wadhamini wa taasisi mbalimbali nchini.

Hata hivyo, wakati CUF upande wa Maalim Seif wakitangaza uteuzi huo wa wajumbe wapya, CUF upande wa Prof. Lipumba nao umeshatangaza kusudio la kuteua bodi mpya ya wadhamini baada ya ile ya awali iliyokuwa ikitambuliwa na Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (Rita) kutenguliwa na Mahakama.

Akizungumza na gazeti hili, Naibu Mkurugenzi wa Habari wa CUF Lipumba, Abdul Kambaya, alisema bodi watakayoiteua itakuwa sahihi kwa mujibu wa sheria na si kwa mujibu wa upande wa Maalim Seif wala Lipumba.

"Bodi tutakayoteua itakuwa sahihi kwa mujibu wa sheria na Rita ndio wataamua bodi sahihi ni ipi na si upande wa Maalim Seif wala Profesa Lipumba watakaoamua," Kambaya alisema.

Nipashe ilimtafuta Naibu Mkurugenzi wa Habari upande Maalim Seif, Maharagande, kutaka kujua juu ya utata wa uteuzi wa bodi hiyo, huku kila upande ukitangaza kuteua bodi yake ambapo mkurugenzi huyo

**INAENDELEA UK. 8**




# Profesa alivyokwamisha kesi ya vigogo wa TPDC

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeshindwa kusikiliza kesi inayowakabili vigogo wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), baada ya shahidi, Prof. Onyango kuugua gafla mahakamani hapo.

Shahidi huyo aliugua ghafla akiwa katika ukumbi namba moja ya mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Kelvin Mhina, muda mfupi baada ya kuingia mahakamani.

Wakili wa Serikali, Aneth Mavika, aliiambia mahakama kuwa shahidi huyo waliyemwandaa anaumwa ugonjwa wa kisukari, hivyo aliiomba mahakama iahirishe kesi hiyo.

Wakili wa utetezi, Mponda Seneni, alidai kuwa hiyo ni mara ya pili upande wa mashtaka unapeleka mashahidi tofauti tofauti hali kama hiyo inajitokeza na kesi inaahirishwa, hivyo aliomba upande wa mashtaka upewe onyo kwa kuwa vitendo hivyo vinajirudia rudia.

Hakimu Mhina alisema upande wa Jamhuri unapeleka mashahidi kwa kuwa kesi hiyo ipo muda mrefu.

Alisema shahidi huyo alifika mahakamani Machi 20, mwaka huu kutoa ushahidi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, James Mataragio, Kaimu Meneja wa Uvumbuzi, George Seni, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Utawala, Wellington Hudson, Mkurugenzi wa Mkondo wa Juu, Kelvin Komba na Edwin Riwa ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Mipango.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa walitenda kosa hilo kati ya Aprili 8, 2015 na Juni 3, 2016.

Ilidaiwa kuwa wakiwa watumishi wa umma na waajiriwa wa TPDC kwa nafasi zao, wakati wakitimiza majukumu yao kwa makusudi walitumia madaraka vibaya.

Ilidaiwa walibadilisha na kupitisha bajeti na mpango wa mwaka wa manunuzi wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016, kwa kuingiza ununuzi wa kifaa cha utafiti cha airborne gravity gradiometer survey ndani ya Ziwa Tanganyika bila ya kupata kibali cha bodi ya wakurugenzi ya shirika.

Ilidaiwa kitendo hicho kinakiuka kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kwa lengo la kujipatia manufaa yasiyohalali ya dola 3,238,986.50 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 7.2 kwa Bell Geospace.

Washtakiwa wapo nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa na mahakama hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Raia wa Peru jela miaka 20 kisa 'unga'

**Na Hellen Mwanga**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imemhukumu raia wa Peru, Wallenstein Santillan, kwenda jela miaka 20, baada ya kupatikana na hatia ya kuingiza nchini dawa za kulevya aina ya Cocaine gramu 1,420.78.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Winfridar Koroso baada ya kusikiliza mashahidi 10 wa Jamhuri bila kuacha shaka, wamemuona mshtakiwa ana hatia.

"Mahakama hii bila kuacha shaka imemwona mshtakiwa ana hatia na inamhukumu kwenda jela miaka 20, ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hiyo," alisema jaji katika hukumu hiyo.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Tuli Helela na Kija Luzingana, uliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa.

Kweka alidai, kwa kuwa mahakama imemwona mshtakiwa ana hatia itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wageni wenye tabia ya kugeuza Tanzania kama daraja la kupitishia biashara haramu.

Wakili wa utetezi, Abbriat Kivea, aliomba mahakama imwonee huruma mshtakiwa ana familia inamtegema na kwamba anajutia kosa lake.

Jaji alisema mshtakiwa atakwenda jela kutumikia kifungo hicho ili iwe fundisho kwa wengine.

Katika kesi ya msingi ilidaiwa kuwa Novemba 16, 2017, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, mshtakiwa alitua kwa ndege ya Emirate akitokea Brazil.

Ilidaiwa aliingia nchini kwa kutumia hati ya kisafiria yenye namba za usajili 116829140 iliyotolewa na Peru.

# Mashahidi mikoani kujenga kesi kigogo Takukuru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa na Jamhuri katika kesi inayomkabili mhasibu mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai, na wenzake kwamba imepokea kibali cha kuita mashahidi kutoka mikoani.

Gugai na wenzake wanakabiliwa na mashtaka ya kughushi, kutakatisha fedha na kumiliki mali za Sh. bilioni 3.6 zisizolingana na kipato chake. Kesi hiyo ilitajwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Wakili wa Serikali, Vitilis Peter, alidai kwamba kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikiliza na Jamhuri waliomba kibali cha kuwaita mashahidi kutoka mikoani, lakini amepata taarifa kuwa kibali hicho kilitolewa jana.

Alidai ili shahidi aweze kutoa ushahidi akiwa anatokea mkoani, ni lazima kipatikane kibali kwa sababu atatakiwa kulipwa.

Wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, aliuomba upande wa Jamhuri kuwataja mashahidi wanaotarajia kuwaita ili kuweka kumbukumbu kwamba asipokuja mmoja aletwe shahidi mwingine.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Peter, alidai hawawezi kutaja majina ya mashahidi hao, ila mahakama itambue kuwa mashahidi watatu wanatokea Mwanza na mmoja anatoka Musoma.

Hakimu Simba alisema upande wa Jamhuri wapeleke mashahidi mahakamani hapo ili kesi hiyo iweze kuendelea na pande zote mbili zipate haki.

Upande wa Jamhuri umeshaita mashahidi sita akiwamo Msajili wa Hati Msaidizi, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Joanitha Kazinja.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Gugai na wenzake wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilimo cha parachichi ni fursa, ichangamkiwe

**ZAO** la parachini limeonekana kupendwa na watu wengi kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini. Lakini pia zao hilo linahitajika katika soko la nje ya nchi.

Mahitaji ya parachichi katika soko yamesababisha bei yake kupaa kila uchao, hivyo kuwa fursa kwa wazalishaji wake, ambao sasa ni tegemeo la kutosheleza nchi nzima. Katika Jiji la Dar es Salaam kwa mfano, kwa sasa kuna uhaba wa bidhaa hiyo, hali inayosababisha parachichi moja liuzwe kati ya shilingi 1,500 hadi shilingi 2,000.

Zao hilo kuwa fursa mpya, ni habari njema kwa wakulima nchini kuitumia kwa ajili ya kuongeza kipato na kupaa kiuchumi kwa ujumla. Ni neema hasa kwa wakazi ambao zao hilo linastawi.

Uzoefu unaonyesha parachichi kustawi katika mikoa yenye hali ya hewa ya ubaridi. Hivyo ni wakati sasa kwa wakazi wa maeneo yenye hali ya hewa ya baridi kujitosa kusaka fursa ya kuzalisha parachichi kwa kuwa ni zao lenye soko kubwa na lenye uhakika kwa sasa.

Jambo la kufurahisha ni kuwa uzalishaji wake hauna gharama kubwa kama yalivyo baadhi ya mazao na vile vile linachukua miaka michache kwa mkulima kuanza kunufaika.

Aidha, hiyo ni fursa kwa wawekezaji wakubwa wa nje na ndani kujitosa katika uzalishaji wa parachichi ili wanufaike na nchi yetu inufaike kwa kodi na ajira kwa wananchi.

Vijana ambao wanasotea ajira wanaweza kuitafutia ufumbuzi changamoto hiyo kwa kujitosa katika kilimo cha parachichi, na hilo linawezekana kwa wale wanaojitambua.

Wanaweza kutumia fursa ya mikopo katika mifuko ya wanawake na vijana katika halmashauri zao, hivyo jambo la msingi ni kwa serikali kuwawezesha kwa kuzipatia maelekezo halmashauri ambazo maparachichi yanastawi kuwapa kipaumbele maalum cha kuwajengea uwezo.

Jambo la msingi ni kwa serikali kuona fursa hiyo na kuipa kipaumbele; kwa maana ya kuhamasisha wananchi kuchangamkia kilimo cha parachichi pamoja na kuwahamasisha wawekezaji.

Kadhalika, kuweka mazingira mazuri ya kilimo hicho. Hata hivyo, baadhi ya hatua zilizoanza kuchukuliwa na serikali zinaashiria kuwa imeona fursa hiyo na kuanza kuichangamkia.

Ziara iliyofanywa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, mkoani Mbeya wiki hii inadhihirisha ukweli wa nia hiyo.

Wakiwa katika ziara hiyo, mawaziri hao walisema kuwa serikali inakusudia kuimarisha kilimo cha maparachichi ambayo yana soko kubwa kimataifa ili kuongeza kiwango cha uuzaji wa bidhaa nje ya nchi utakaosaidia kuongeza pato la taifa.

Katika ziara hiyo iliyokuwa na lengo la kutatua changamoto za wawekezaji wa zao hilo. Waziri Mpango alisema moja ya kigezo cha kukua kwa uchumi ni namna nchi husika inavyouza bidhaa zake kwenye soko la kimataifa, hivyo akasisitiza kuwa parachichi ni miongoni mwa mazao yatakayoifanya Tanzania kufikia hatua hiyo.


Alisema wawekezaji wakubwa wa maparachichi katika Wilaya ya Rungwe yaani kampuni za Rungwe Avocado Limited na Cuser Africa Limited, zimeleta fursa kubwa ambazo wananchi wanatakiwa waitumie kuinua uchumi wao na wa taifa. Alisema serikali inataka zao la parachichi liwe miongoni mwa mazao yanayouzwa nje, hivyo inawahamasisha wananchi waitumie vizuri fursa hiyo.

Naye Kairuki alisema ofisi yake inawakaribisha wawekezaji wengine kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza ushindani. Ni matarajio yetu kuwa zao hilo litapewa kipaumbele na taasisi za utafiti ili liisaidie nchi katika kukuza uchumi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Mauaji Njombe yatukumbushe umakini kulinda watoto wetu

Na Yasmine Protace

**NI** hivi karibuni yametokea mauaji ya watoto mkoani Njombe, yakidaiwa chanzo ushirikina.

Nami katika kauli yangu kujibu msimamo papo kwa hapo nasema; ushirikina ukomeshwe na usipewe mwanya, kwa wote wenye azma ya kuendeleza matukio ya namna hiyo, si Njombe tu, bali nchi nzima.

Huko Njombe, watoto waliokumbwa na mkasa ni binadamu wenzetu waliokuwa katika mchakato wa kujenga maisha yao, wakiwa katika ndoto zao zinazoungwa mkono na wazazi au walezi, baada ya kumaliza shule. Walitarajia kuwa watu wa aina fulani kulitumikia taifa lao.

Inasikitisha kwamba watoto hao hawakufikia ndoto zao, kwa sababu ya makusudio ya wengine walioibuka na dhamira za kukatiza maisha yao.

Sote tukumbuke na kuzingatia kuwa, watoto wana haki kama wengine na utoto wao usigeuke kigezo cha kukatisha maisha yao.

Pia, tunajua namna serikali ilivyostushwa na kilichotokea kwa jinai hiyo, dhidi ya watoto tuwapendao.

Mbali na kutuma timu ya wana usalama, iliunda tume ya kuchunguza mzizi wa mauaji ya Njombe, ili kupata mtazamo bora dhidi ya namna wanavyoweza kukomesha matukio hayo.

Tukipanua mbali mtazamo wa kilichotokea Njombe, historia ina nyayo za mauaji ya watoto katika baadhi ya mikoa, moja ya sababu ni imani za kishirikina na ugomvi kati ya wazazi.

> **Tukipanua mbali mtazamo wa kilichotokea Njombe, historia ina nyayo za mauaji ya watoto katika baadhi ya mikoa, moja ya sababu ni imani za kishirikina na ugomvi kati ya wazazi.**

Ni hoja zisizo na mashiko kisaikolojia, imani za kidini, mbele ya sheria na haki za binadamu. Ni ukatili unawakatishia watoto haki zao za kuishi na ndoto walizo nazo.

Katika mauaji ya Njombe, taasisi ya TGNP Mtandao, kwa kushirikiana na wadau wa haki za wanawake, haki za watoto na usawa wa kijinsia, walitoa salamu za rambirambi kwa familia zilizofikwa na majanga hayo, wakiwamo wazazi na walezi waliopoteza watoto.

Ni salamu zilizoendana na tamko linalolaani ukatili dhidi ya watoto, kwamba ni jambo lisilovumilika, kwa kuwa wajibu wa mzazi, mlezi na mtu mzima yeyote ni kuwalinda watoto hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, anafafanua kuwa vitendo hivyo havikubaliki katika jamii, kwa sababu ni kinyume cha Azimio la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu la tarehe 10 Desemba 1948, akinukuu kifungu kimojawapo kuwa: "Kila mtu ana haki ya kuishi, haki ya uhuru na haki ya kulinda nafsi yake."

Bosi huyo wa TGNP, anarejea Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, inavyotamka haki hiyo, sambamba na Sheria ya Haki ya Kuishi ya Mwaka 1984.

Anasema jamii ina wajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya ukatili wa kijinsia, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), unaolenga kupunguza nusu ya ukatili uliopo dhidi ya wanawake na watoto katika jamii, ifikapo mwaka 2022 au miaka mitatu ijayo.

Kilio cha Lilian ni kwamba, matukio yanasababisha vifo vya wananchi (wanawake, wanaume, wazee na watoto) wasio na hatia, akitoa mfano mbali na watoto, ni mauaji ya vikongwe na wenye ualbino.

Anasema TGNP Mtandao, inatambua jitihada za serikali katika kila ngazi ya jamii, inavyokabiliana na uhaini huo, mfano hai ni kuundwa kamati ya kuchunguza mauaji ya Njombe.

Lilian anahimiza serikali kupitia vyombo vyake, visimamie Sheria ya Kudhibiti Uchawi ya Mwaka 1998, inayoagiza udhibiti wa ushirikina na anatumia fursa hiyo kuiasa jamii, kutoa ulinzi wa mtoto, pia kushirikianan na wadau wake kuzijengea uwezo kamati za ulinzi wa watoto.

## BARUA/MJADALA

## Tuboreshe pa kuangalia soka

**Mhariri,**

*HIVI sasa ushabiki wa mpira katika maeneo mbalimbali umetawala kila kona nchini. Ni kawaida, kuna sehemu mbalimbali zimejaa kumbi za kushuhudia mipira kwa njia ya runinga.*

*Ni aina mpya ya burudani iliyowashika watu wakashabikia katika kila namna wanavyopenda, ili mradi inakuwa ni ulingo wa burudani kwa umma, katika maeneo mbalimbali.*

*Kimsingi, ni namna ya kuunganishwa na dunia, kwa kuwa ndio burudani ya soka la dunia ililotawala nchi zote, huku nchini pia kukiwapo michezo ya nyumbani.*

*Aina hiyo ya starehe, imeshamiri mwanzo katika baa, sasa imezidi kutanuka watu kuunda sehemu za kuangalia mpira katika kumbi maalum.*

*Hiyo si mijini tu, bali hata vijijini nako mambo yameshamiri sana kuhusiana na kumbi za kuangalia michezo ya soka, ambako wakazi wake wameamka na wanaenda sawia na wenzao wa mjini kuhusiana na uelewa wa mambo mbalimbali.*

*Huu ni ujumbe mzuri, ila kunatakiwa sasa tupige hatua zaidi, kwamba katika maboresho ya sehemu hizi za kuangalia mpira ziwekwe za kisasa zaidi kukidhi matakwa yanayotakiwa na waangaliaji mipira.*

*Ikiangaliwa kwa kina, kumbi hizi zinachukua nafasi ya kilichokuwapo katika zama zilizopita, katika miji mikubwa kulikuwapo kumbi za sinema watu walifurahishwa sana, mathalani Dar es Salaam, kulikuwapo kumbi kama Avalon, New Chox, Odeon, Cameo, Empress, Empire zilizokuwa katikati ya jiji.*

*Pia, nje ya jiji kulikuwapo ukumbi wa Drive Inn, ambao ulikuwa wa aina yake watu waliingia na magari yao na kulikuwapo na bango refu. Hivi sasa mahali hapo ni ofisi za ubalozi mmojawapo uliopo nchini.*

*Maboresho ya sehemu za kuangalia soka yanaweza yakafanywa kupitia njia kuu mbili. Moja ni kupitia uimarishaji wa biashara binafsi na ya pili, sera na miongozi kutoka mipango ya serikali za mitaa nchini.*

**Abbas Theuji,**
**Kibaha.**

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Matapeli wanaovizia pesa za simu ‘pasua kichwa’




**Na Sabato Kasika**

MATAPELI wanaotumia watu mbalimbali ujumbe wa maandishi wa: ‘Ile pesa itume kwenye namba hii,” sasa wamerudi kwa kishindo, siku chache tangu walipotangaziwa vita na vyombo vya dola, huku baadhi yao wakiwa wametiwa mbaroni.

Jeshi la Polisi lilianza msako dhidi ya matapeli hao Juni mwaka jana, na kuwafanya Watanzania kupumua kidogo.

Hadi sasa wana - usalama hao kwa kushirikiana na asasi za mawasiliano ya simu wanatumia ujumbe wa kila mara kuielimisha jamii dhidi ya utapeli huo.

Ni hali inayoonekana imerudi kwa kasi. Haipiti wakati au siku, bila ya simu ya mtu kupata ujumbe wenye hoja hizo katika simu za watu mbalimbali.

Mimi niko kwenye kundi hilo, nakumbuka mara ya mwisho ni siku ya Februari 18 mwaka huu, nikipata ujumbe ulioandikwa hivi “sasa hivi nitumie hiyo hela kwenye hii namba 0717 0773... (Charles...) Jitahidi itume sasa hivi. “

Ujumbe huo ulitoka katika simu namba 0712-6915...kimsingi, huo siyo ujumbe wa kwanza kunifikia mwezi huu, bali nimekuwa nikitumiwa kila mara naisoma, kisha ninaifuta mara moja, katika hali ya kuipuuza, ingawaje kuna ukweli kwamba zinakera.

Leo haja ya kukumbushana kuwa matapeli hao bado wapo kazini kama kawaida. Ninaamini kwamba, ujumbe wa aina hiyo utakuwa umetumwa kwa watu mbalimbali, kwa kuwa wapo baadhi niliwauliza, wamekiri kutumiwa ujumbe huo wenye fedheha za kitapeli.

Polisi inajitahidi kutuma ujumbe wa kutahadharisha raia wema kuepuka kuingia kwenye mtego huo, lakini katika sura ya pili, matapeli nao wanashindana kufanikisha uhalifu wao.

Binafsi nimepokea ujumbe wa maandishi kutoka Jeshi la Polisi unaonitaka kuwa makini ninapofanya miamala ya pesa ili isiende kwa matapeli.

Katika mazingira hayo, inawezekana wakawapata watu ambao ni wageni katika mawasiliano ya simu, wakawaibia pesa kirahisi. Hivyo, vyombo vya dola viendelee kuwadhibiti, kwa kuwa mchezo huu haukubaliki.

Hivi sasa, matapeli hao wameingia hatua ya pili, kuwapigia simu watu na kujifanya ni wafanyakazi wa kampuni za simu wanaohitaji kujua salio la fedha, katika akaunti ya simu ya mteja.

Tabu yangu ni kampuni za simu katika nafasi zao wanachukua hatua gani kuwadhibitu matapeli hao. Siamini kama kampuni zetu za simu awe watendaji wake hawazijua namba hizo za watendaji kwa kuwa kuna suala la usajili wa laini zao.

Hivyo, wakati vyombo vya dola vikichukua nafasi yake kudhibiti utapeli, kampuni za simu nazo zihakikishe zinawabana wateja wanaoshiriki uhalifu huo, kwa kuwa bila hivyo, raia wema wenye simu wataendelea kulizwa kila siku.

Wapo watumiaji wapya wengi wa simu wasiojua vizuri mbinu zinazotumiwa na matapeli. Ikumbukwe, kila wakati watu wanafanya miamala ya fedha na matapeli.

Ndio maana, mtu anafanya muamala, ghafla anapata ujumbe unaomwelekeza kutuma pesa katika namba fulani.

Sasa kama atakuwa mgeni wa mambo ya mawasiliano, anaweza kujikuta anatuma pesa kusiko husika, hivyo anakuwa tayari ameshatapeliwa.

Mnajua ndio sababu za polisi wanatumia Watanzania ujumbe unaowataka kuwa makini katika miamala ya pesa, kuepuka uhuni.

Mwaka jana kuna watu waliowasiliana na kupanga kutumiana pesa za biashara, mmoja akiwa Dar es Salaam na mwingine Mbeya.

Walikubaliana wa Mbeya amtumie wa Dar es Salaam pesa na akaenda kwenye kibanda cha huduma ya pesa. Akiwa katika mchakato wa kutuma pesa, ujumbe uliingia katika simu yake ukimtaka atume hiyo pesa katika simu iliotumika kumtumia ujumbe huo.

Bila kuutafakari ujumbe huo, aliituma kisha akamjulisha mwenzake wa Dar es Salaam, tayari ameshatuma. Baada ya nusu saa, mtumaji alihoji kama pesa hiyo zimefika, akaambiwa bado.

Ndipo akageuka mbogo kumwambia mwenzake wa Dar es Salaam ndiye tapeli aliyemtuma ujumbe; “hiyo pesa tuma katika namba hii.”

Huyo wa Dar es Salaam, alikana lawama, hali iliyozua mzozo, aliyetuma akaenda kutoa taarifa kituo cha polisi, akieleza mkasa ulivyo.

Baada ya kuambiwa hivyo ilibidi awe mpole. Hapa ina maana kwamba wanachofanya matapeli hawababahatishi, wanajua wapo baadhi ya Watanzania ambao hawajui lolote kuhusu kinachoendelea na wanaweza kutapeliwa kirahisi, hivyo ni muhimu kuwa makini.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# JPM ateua mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Dk. Michael Wilfred Ng'umbi kuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW). Kabla ya uteuzi huo Dk. Ng'umbi alikuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Kitivo cha Elimu cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Dk. Ng'umbi amechukua nafasi ya Dk. Fidelice Mafumiko ambaye aliteuliwa kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Wakati huo huo, Rais Magufuli amemteua Jaji Stephen Mrimi Magoiga kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Ushindani (FCT).

Jaji Magoiga amechukua nafasi ya Jaji Barke Mbaraka Sehel ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, imeeleza jana kuwa uteuzi wa viongozi hawa ulianza Jumanne.



Watoto wakicheza kwenye mtaro wa maji ya mvua kando ya Barabara ya Shekilango jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mabilioni ya Barrick kutua Machi

**INATOKA UK. 2**

kitakachokuwa tofauti na makubaliano yaliyofikiwa awali ambayo yaliongozwa na Mwenyekiti Mtendaji wa Barrick Gold Corporation, Prof. John Thornton, ikiwemo Barrick Gold Corporation kuilipa serikali ya Tanzania kifuta machozi cha Dola za Marekani Milioni 300 (sawa na Sh. Bilioni 682.5).

Makubaliano mengine ni kuendelea na uwekezaji kwa ubia kati ya serikali ya Tanzania na Barrick Gold na mgawanyo wa mapato ya kiuchumi kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50 kati ya Tanzania na kampuni hiyo.

Taarifa hiyo ilisema Dk. Jacobs alimpongeza Rais Magufuli kwa jitihada zake za kusimamia maslahi ya Watanzania katika rasilimali za nchi na kwamba pamoja na ukweli kwamba Rais yuko katika njia sahihi, akiwa Mwafrika anaunga mkono juhudi hizo kwa kuwa ndio mwelekeo sahihi ambao nchi za Afrika zinapaswa kuufuata.

"Mimi ni Mwafrika na sisi sote ni Waafrika. Anachokifanya Rais Magufuli ni sahihi kabisa, anahakikisha utajiri wa rasilimali uliopo unabainishwa na unawanufaisha Watanzania ndiyo maana tupo hapa kwa sababu tunakubaliana na Rais," alisema kama alivyokaririwa na taarifa hiyo.

"Na hivi ndivyo sisi Waafrika tunapaswa kufanya kwa rasilimali zetu, na sisi tunahakikisha tunafanya kazi vizuri na serikali na jamii kulinda rasilimali hizi, kumbuka rasilimali hizi ni za wananchi, jukumu langu kama mwekezaji ni kubadili hayo madini kuwa kodi na ajira kwa Tanzania na pia kampuni yangu kupata faida yake halali," aliongeza.

Alibainisha kuwa baada ya muungano huo wa Rand Gold na Barrick Gold, sasa kampuni mpya ya Barrick Gold imekuwa kubwa inayoongoza kwa umiliki wa rasilimali za dhahabu duniani ikimiliki rasilimali tano kati ya 10 na kwamba kutokana na uwezo huo, Barrick Gold Corporation sasa imejiimarisha zaidi kiuwekezaji na utaalamu na iko tayari kushirikiana na Tanzania kuhakikisha dhahabu iliyopo inaleta manufaa kwa pande zote mbili yaani Watanzania na mwekezaji.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, ambaye aliongoza timu ya majadiliano kwa niaba ya serikali ya Tanzania na Barrick Gold, alisema nyaraka za makubaliano hayo zimekamilika na kwamba kinachosubiriwa ni utekelezaji wa unaotarajiwa kukamilika ifikapo mwisho wa Machi, mwaka huu.

"Baada ya muungano wao (Rand Gold na Barrick Gold Corporation) hii sasa ni timu mpya na tumewaona ni watu ambao sasa wako tayari kutekeleza yale yote yaliyokubaliwa. Sasa ni kwa kila upande kwenda kwenye vyombo vyake vinavyohusika kufanya uamuzi wa mwisho ili utekelezaji ufanyike," alisema Kabudi.

## Serikali yaita wanunuzi binafsi korosho

**INATOKA UK. 2**

viwanda vya ndani vitapata korosho ghafi za kutosha na kwa lengo la kujiandaa vizuri msimu ujao wa uzalishaji, imepanua wigo kwa kukaribisha wanunuzi zaidi.

Alisema wanunuzi hao wenye maduka makubwa, wamiliki wa viwanda wenye nia ya kusafirisha sehemu mbalimbali duniani na wanaotaka kununua na kuzihifadhi ili baadaye wabangue kwa utaratibu wao, pia wanakaribishwa kupeleka maombi kwa kiasi chochote wanachohitaji.

Pia alisema wanunuzi hao lazima watambue kuwa korosho hizo zimenunuliwa kwa Sh. 3,300 kwa kilo na kuna gharama za usafirishaji kutoka shambani hadi kwenye chama cha msingi, gharama za kusafirisha kutoka chama cha msingi hadi ghalani, gharama za upakiaji na upakuaji.

Alitaja gharama nyingine ni za kuhifadhi kwenye maghala, magunia, malipo ya vyama vya ushirika, tozo za kisheria zikiwamo za halmashauri na gharama zingine zikiwamo kuchangia elimu.

## Maalim Seif ateua wajumbe 9 wa bodi

**INATOKA UK. 4**

alisema wao wako sahihi kisheria.

"Ukisoma vizuri hukumu ya mahakama utaelewa kila kitu na pia katika taarifa niliyoitoa kwa vyombo vya habari na mitandao," Maharagande alisema.

Katika taarifa aliyoitoa mkurugenzi huyo iliyosambaa katika mitandao ya kijamii licha ya kutaja majina ya wajumbe wapya wa bodi hiyo imeeleza hoja 11 alizodai kutolewa na Mahakama Kuu na kusababisha kufutwa kwa bodi hiyo na mahakama.

Alipoulizwa iwapo bodi hiyo mpya iliyoteuliwa haita tambuliwa na (Rita) kama ambavyo ilikuwa mwanzo, Mkurugenzi huyo alisema watachukua hatua kwa kufanya vikao vya chama kuona hatua gani za kuchukua.

"Kwa sasa siwezi kuongelea hilo ila likitokea tuna vikao vya chama vya kuamua," alisema Maharagande.

Wakati hayo yakiendelea, kesi nyingine inayokihusu chama hicho kuhusu uamuzi wa kumtambua Prof. Lipumba kama Mwenyikiti halali ama la unasubiriwa kwa hamu na wafuasi wa pande zote mbili ifikapo Februari 22 mwaka huu.

"Tukutane tena Mahakama Kuu tarehe 22 Februari 2019, siku ya Ijumaa. CUF mpya, CUF moja, CUF imara, CUF yenye nguvu inaenda kurejeshwa katika mstari wake," alisema Maharagande.

## HABARI KITAIFA

# Unyang'anyi wamkera PM kwenye maeneo mipakani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuongeza ulinzi na doria katika maeneo ya mipaka kutokana na ongezeko la vitendo vya mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha na vitisho kwa wananchi.

Pia, Waziri Mkuu ameagiza wakimbizi wote watakaobainika kutoroka kwenye makambi wanayohifadhiwa na kuingia uraiani wakamatwe na wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria za Tanzania, kwa kuwa wanachokifanya ni ukiukwaji wa sheria.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo juzi jioni alipozungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara kwenye Uwanja wa Taifa wilayani Kibondo, wakati akihitimisha ziara yake mkoani Kigoma.

Alisema maeneo yaliyo katika hali mbaya ni Kibondo, Buhigwe, Kasulu, Ngara, Biharamulo, Uvinza, Kakonko na Kigoma Vijijini, ambako wananchi hususan wafanyabiashara wameingiwa na hofu kutokana na vitendo hivyo.

Waziri Mkuu alisema pamoja na undugu waliokuwanao na nchi jirani, lakini kila nchi ina sheria na taratibu zake, hivyo ni lazima zifuatwe na ni marufuku kuingia katika nchi yoyote bila ya kufuata sheria na taratibu za nchi husika.

"Kulinda usalama wa nchi ni jukumu letu sote na si la vyombo vya ulinzi na usalama pekee, kila mmoja anapaswa kushiriki. Kwa upande wa majirani zetu wanaotaka kuja nchini ni lazima wafuate utaratibu kwa kuomba vibali."

Alisema watu wote wanaoingia bila ya kufuata sheria na taratibu ndio hao wanashiriki katika vitendo vya uhalifu yakiwamo mauaji ya raia wasiokuwa na hatia, unyang'anyi wa kutumia silaha za kivita pamoja na utekaji wa watoto.

Waziri Mkuu alisema vyombo vya ulinzi na usalama viendelee kulinda mipaka na watu wote watakaobainika wameingia nchini bila vibali wakamatwe na wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

Aliongeza kuwa wakimbizi wanaohifadhiwa katika maeneo mbalimbali nchini hawaruhusiwi kutoka nje ya kambi hizo kwa sababu huduma zote wanazostahili zikiwamo za afya, elimu na chakula zinapatikana kambini.

Pia, aliitaka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iwasimamie vizuri watumishi wake wanaofanya kazi kwenye kambi hizo na kuchukua hatua kwa watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Mbali na agizo hilo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, pia Waziri Mkuu aliutaka uongozi wa wizara hiyo ufanye mazungumzo na Shirika la Kuwahudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) ili litekeleze majukumu yake bila kukiuka sheria za nchi.

Kadhalika, aliwaonya wananchi kuacha tabia ya kuwachukua raia wa nchi jirani na kuwaleta nchini kwa ajili ya kufanya kazi za vibarua katika mashamba yao bila ya kuwa na vibali.

"Tabia ya kuwachukua watu kutoka nchi jirani kwa ajili ya kulima mashamba bila ya kuwaandikisha ni makosa kisheria. Anayetaka kupata vibarua kutoka huko aende kuomba vibali, huku akieleza idadi ya anaowataka na siku watakazokaa."

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kulinda usalama kwa sababu wengine wanawafanyisha kazi na wakimaliza hawawalipi wanawatishia kuwashtaki kwa kuingia nchini bila ya kibali jambo linalochangia kuwapo kwa migogoro na visasi.

Vilevile, Waziri Mkuu alisema hata kama wakiwalipa hakuna anayefuatilia kama kweli baada ya kumaliza vibarua hivyo wanarudi makwao kwa kuwa wengi wao wanaendelea kubaki nchini, huku baadhi wakijihusisha na vitendo vya kihalifu.



Daktari bingwa wa afya ya kinywa na meno kutoka Malaysia, Dk. Rajamani akielezea faida ya kutumia virutubisho vya Stemregen katika mwili wa binadamu kwenye semina ya uzinduzi wa matumizi ya virutubisho hivyo, kutoka Marekani jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanaohamishwa Msimbazi kulipwa fidia

**Na Elizabeth Zaya**

JIJI la Dar es Salaam limesema litawalipa fidia wakazi wote watakaohamishwa kutoka Bonde la Mto Msimbazi kupisha mradi wa uboreshaji wa jiji hilo unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Ofisa Mipango Miji wa jiji hilo, Grace Mbena, aliiambia Nipashe juzi kuwa, tayari wameshafanya mazungumzo na wakazi hao kuhusu namna watakavyolipwa fidia.

Mbali na kulipwa fidia, Mbena pia alisema wakazi hao watapewa kipaumbele zaidi katika miradi itakayoanzishwa kwenye eneo hilo ambalo limekuwa likifurika maji kipindi cha mvua.

"Mbali na kuwalipa fidia, kuna miradi mingi ambayo itaanzishwa katika eneo hilo ikiwamo ujenzi wa makazi ya kisasa, lazima tutahakikisha wao wanapewa zaidi kipaumbele," alisema Mbena.

Alisema jumla ya Dola za Marekani milioni 120 (Sh. bilioni 279) zimetolewa na Benki ya Dunia (WB) pamoja na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) kwa ajili ya mradi huo.

"Jiji la Dar es Salaam limejipanga kuimarisha miundombinu ya Bonde la Mto Msimbazi kwa kujenga miundombinu upya na ili kukamilisha mkakati huo, limeandaa utaratibu mzuri wa kuwahamisha wananchi walioko pembezoni ya mto huo. Mpango wa kuwaondoa umeshakamilika na kazi itaanza wakati wowote kuanzia sasa," alisema Mbena.

# Kibano kikali kwa madiwani wa CCM

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Ally Msikamo, amesema kuwa madiwani wa wilaya hiyo wasioshiriki kutatua kero katika kata zao wajiandae kuhojiwa na ofisi za CCM.

Hayo yalisemwa na Msikamo katika kikao cha Baraza la Madiwani na kupitisha bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 30 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Msikamo alisema amefanya ziara katika kata mbalimbali za Mkuranga, lakini katika ziara hizo wananchi walalamikia baadhi ya madiwani kuwa hawaendi katika kata kushughulikia kero za wananchi.

"Mmechaguliwa na wananchi, lazima mtatue kero zao, kama mtashindwa hata kufika vijijini na kutatua kero, tutawaita madiwani katika ofisi za chama na kuwahoji," alisema.

Aliongeza kuwa kila diwani anatakiwa kusimamia ilani ya chama tawala ili kuleta maendeleo kwa wapigakura na kutojali itikadi za vyama.

Alifafanua zaidi kwamba ataendelea kufanya ziara kila kata na kama akikuta malalamiko ya diwani kutoshirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo, ataitwa ofisi za chama na kuhojiwa.



Makamu Mwenyekiti wa chama kikuu cha ushirika wa mkoani Shinyanga (SHIRECU), Enock Lyeta (wa pili kulia), akikagua ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Shule ya Sekondari Buluba, inayomilikiwa na chama hicho, iliyopo mjini Shinyanga juzi. Kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Frednand Chuwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wito kuchangamkia fursa soko la Ukraine

**Na Elizabeth Zaya**

WATANZANIA wametakiwa kuzalisha kwa wingi bidhaa za kilimo ikiwamo kahawa, chai na viungo mbalimbali ili kuchangamkia fursa ya soko ambalo limepatikana Ukraine.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam Kaimu Meneja Mpango na utafiti wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), John Fwalo, alisema soko kubwa la kuuza bidhaa mbalimbali nchini Ukraine limepatikana na wameomba Watanzania kwenda kuuza bidhaa hizo nchini humo.

Fwalo alisema katika kuchangamkia soko hilo, wameanza kutoa semina kwa wakulima nchini ili kujua namna gani watakavyozalisha bidhaa bora za kutosha kwa ajili ya kwenda kuziuza katika nchi hiyo.

"Kwa hiyo jambo jingine tunalolifanya ni kutambua wadau wa kilimo wanaozalisha bidhaa hizo, ili kuwaandaa kwa ajili ya kuchangamkia fursa hiyo, kwa ujumla bidhaa zinahitajika kwa wingi sana kutoka Tanzania, ni sisi tu kuchangamka," alisema Fwalo na kuongeza:

"Mbali na bidhaa hizo, lakini pia tumeambiwa bidhaa nyingine zinazohitajika katika soko hilo la Ukraine ni za viwanda. Sisi Watanzania tunauza sana bidhaa za chai na kahawa katika soko la Ulaya, lakini kwenye bidhaa mpya kama za viungo kidogo ni vigeni kwetu, hatujawa na uwezo wa kuongeza thamani, kwa hiyo wao watakuwa wananunua mbegu na kwenda kuongeza thamani." Alisema hali ya biashara kati ya Ukraine na Tanzania kwa sasa iko vizuri na kwa kipindi cha mwaka 2016, 2017 na 2018, ilionyesha kwamba ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo unakua.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wasindikaji (Tafopa), Suzi Laizer, alisema ni wakati mwafaka kwa wakulima kuunganisha nguvu ya pamoja kuchangamkia fursa hiyo.

"Tunashukuru kwa kupatikana kwa soko hili na tumeambiwa soko ni kubwa sana, mimi ninachoomba ni kwa wakulima tusizubae, tupambane kulichangamkia. Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo waandae wakulima kwa ajili pia ya zao la 'export' (kusafirisha nje) kwa sababu katika upande huo bado hatuko vizuri na wakifanya hivyo watakuwa wametusaidia sana," alisema Laizer.

# Maofisa wa afya mpakani washauriwa kuhusu ebola

**Restuta Damian,** MISSENYI

MAOFISA afya wa mpaka wa Mtukutula kati ya Tanzania na Uganda uliopo wilayani Missenyi mkoani Kagera, wametakiwa kuwa na uhusiano wa karibu na vyombo vya habari kwa ajili ya kupeana taarifa za afya ukiwamo ugonjwa wa ebola.

Akizungumza na makundi hayo msimamizi wa vituo vya afya mipakani kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Remigius Kakulu, alisema kuwaweka pamoja ni kutaka kusaidia jamii kupata elimu juu ya ugonjwa wa ebola.

Kakulu alisema kuwa, Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa ya Katavi, Kigoma, Mwanza, Songwe, Dar es Salaam na Rukwa, ambayo kuna uwezekano wa kukumbwa na ugonjwa wa ebola.

Aidha, Kakulu alisema kupitia vyombo hivyo, wananchi wa mkoa huo wanapaswa kupewa elimu ya tahadhari, kutambua dalili za ugonjwa huo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), inayoripotiwa kuwa na wagonjwa 800 kwa mwezi, huku watu 200 wamekwisha fariki dunia.

"Kikubwa hapa ni uhusiano mzuri wa kupeana taarifa kwa jamii yetu ya mkoa Kagera na mikoa inayopakana na nchi jirani zaidi ya mbili na DRC ndiyo yenye ugonjwa. Kuna uwezekano mkubwa wa raia wa nchi hiyo kuingia hapa na asijulikane," alisema.

Mganga Mkuu Hospitali ya Missenyi, Hamis Abdallah, alisema tangu kuripotiwa ugonjwa huo, timu ya maofisa afya imeweka taratibu za kufanya upimaji kwa kutumia vifaa maalum vya kisasa.

# RPC mpya awapa salamu wahalifu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KAMANDA mpya wa Polisi mkoani Mwanza, Muliro Jumanne, ametangaza vita dhidi ya wahalifu sugu watakaojaribu kuwarushia risasi askari ambao watakuwa wakitekeleza majukumu yao.

Aidha, ameahidi kuendeleza mapambano makali yaliyokuwa yakifanywa na mtangulizi wake, Jonathan Shanna, aliyehamishiwa makao makuu ya Jeshi la Polisi, huku akiwaomba wananchi kuendeleza ushirikiano wao wa kutoa taarifa bila kuwa na shaka.

Muliro aliyasema hayo jana, kwenye makabidhiano ya ofisi na Kamanda Shanna ambaye amehamishiwa kitengo cha operesheni maalumu.

Muliro alisema mambo aliyoyaanzisha na kuyatekeleza Shanna atayaendeleza kwa kasi na kuyaboresha zaidi kwa lengo la kuhakikisha usalama unaendelea kuwapo kwa wananchi wake, hivyo waendelee kufanya shughuli zao za kila siku za kukuza uchumi wa bila hofu.

"Shughuli kuu za jeshi hili ni kulinda raia na mali zao, ninachokifanya ni kuhakikisha ninaboresha mfumo wa kushughulikia wahalifu hasa sugu kwa lugha nyingine majambazi na wote wanaojihusisha na vitendo hivyo, kuhakikisha vinakomeshwa kwa asilimia kubwa kama sio kuisha kabisa," alisema Muliro.

Muliro aliwaomba wananchi wa mkoa huo, kuendelea kuliamini jeshi hilo kwa kulitumia vizuri kwa kutoa taarifa muhimu dhidi ya viashiria vyovyote vinavyoonyesha uvunjifu wa amani ili hatua zichukuliwe mapema.

Kwa upande wake Kamanda Shanna akitoa neno la kuaga, alisema, Kamanda Muliro ni mzoefu, mwadilifu, mchapa kazi, hodari na amefanya kazi katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Mimi naondoka, lakini vikosi kabambe, vyenye weledi wa hali ya juu, vikosi jasiri vinabaki hapa mkoani, kwa hiyo ulinzi haujahama uko wa kutosha na wanaotaka kujaribu uhalifu wajiandae kutembezewa kichapo, kwa kuwa askari wapo makini na wapo tayari kulinda amani ya raia na mali zao," alisema Shanna.

Alimalizia kwa kusema kauli mbiu yake haitabezwa kwa sababu moto kwa wahalifu ndio umewashwa.

HABARI ARUSHA

# Wadau wa tanzanite waipongeza serikali kufuta leseni za raia wa nje

**Na Mwandishi Wetu**, ARUSHA

WALIOKUWA wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite na baadaye kuporwa mgodi wao katika mazingira tatanishi, wameipongeza serikali ya Rais John Magufuli kwa kuwafutia leseni ya uchimbaji raia wa Kenya, ambao walikuwa wakifanya kazi hiyo Mirerani.

"Ni sahihi kabisa, serikali imefanya kazi kubwa (serikali hii ya Magufuli). Tumeteseka na hao raia wa nje robo karne sasa, tumehangaika sana na huyu mtu raia wa Kenya aliyepora mgodi wetu mwaka 1995.

"Anapaswa kufukuzwa nchini sasa, lakini kabla ya hatua hiyo uchunguzi dhidi yake ufanyike kwa kina ili kubaini ufisadi alioufanya katika uchimbaji wa tanzanite kwa muda wote huo," alisema Omari Said Bikubi ambaye kwa sasa ni kipofu.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumatatu wiki hii mjini Dodoma, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alitangaza kuzifutia leseni kadhaa zikiwamo za raia wa Kenya ambazo ni zenye namba PML003227/NZ, PML003387/NZ. Aidha, alisema maombi yake ya namba PML12823/NZ, PML13036/NZ, PML23159/NZ, PML25398/NZ, PML25786/NZ na PML25789/NZ yapo katika hatua mbalimbali ya kupatiwa leseni kinyume cha sheria. Waziri ameiagiza Tume ya Madini nchini kuwachukulia hatua walioshiriki kutoa leseni hizo.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Madini, kinakataza leseni ndogo za uchimbaji kutolewa kwa wageni.

Mapema Bikubi na mwenzake Thadei Joseph Mtingange, wakizungumza jijini hapa jana, walisema walikuwa wanamiliki mgodi namba 145 na mwenzao Abubakar Saleh Mwamba, lakini katika mazingira yasiyoeleweka mgogoro ulizuka kati yao na Anthony Ngoo ambaye ni raia wa Kenya kuhusu umiliki wa mgodi huo.

Bikubu alisema Ofisi ya Madini Kanda ya Arusha, kupitia barua yake ya Machi 21, 1995, kwenda kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usuluhishi, Kitalu D, Mirerani, iliafiki uamuzi uliofikiwa na kamati hiyo kuwa Mfinange aendelee na uchimbaji katika mgodi huo.

"Ndugu Anthony Ngoo ambaye ameelezwa kuwa alikuwa mfadhili wa Mfinange hakustahili kulipia mgodi huo kama alivyofanya," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Aidha, ofisi hiyo iliandika barua nyingine, Juni 6, 1995 kwenda kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usuluhishi, Kitalu D, Mirerani, ikimtaja Mfinange kuwa ameshalipia mgodi huo na ofisi ilikuwa inaandaa hati kwa ajili yao ambayo wangeipata baada ya muda mfupi.

Aidha, barua hiyo iliitaka kamati ya ulinzi na usuluhishi kuhakikisha watu wote waliopo katika shimo hilo wanaondoka ili Mfinange na wenzake waweze kuanza kazi hapo bila bughudha. Lakini walisema katika mazingira yenye utata, kabla ya kupata hati ambayo walikuwa wamekwishalipia, walijikuta raia huyo wa Kenya akiwa tayari ameshapewa leseni ya kuchimba na wao kuwekwa kando.

Walisema awali raia huyo wa Kenya alikuja na kufanya kazi za udalali wa kununua madini huko Mirerani na alikuwa akidai kuwa ni Mtanzania.

"Unajua wakati huo kule Mirerani mambo yalikuwa yakifanyika kienyeji tu, watu wanaingia na kuchimba madini ovyo ovyo," anasema Mfinange. Lakini kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyoandaliwa na Idara ya Uhamiaji Juni 11, 1996, ilisema Anthony Ngoo alikuwa akiishi nchini kinyume cha sheria, na alifikishwa mahakamani kwa kosa hilo baada ya kukamatwa na maofisa hao.

Walisema tangu wakati huo hawakukaa kimya, isipokuwa walichukua hatua kadhaa kulalamikia suala hilo katika ngazi mbalimbali hadi wizarani na wanaipongeza serikali ilichukua maamuzi yenye maslahi mapana kwa taifa.

"Tunaishukuru Wizara ya Madini kwa kumfutia leseni huyu raia wa Kenya, tunaomba sasa achukuliwe hatia zingine za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani na kufukuzwa nchini," alisema Bikubi.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, akizungumza mbele ya mawaziri saba waliofika kusikiliza mgogoro wa ardhi kati ya vijiji vya Kimotorok, Irkushbor, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Pori la Akiba la Mkungunero, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wajawazito sasa wapata ahueni ya umeme wa jua

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KATIKA kuhakikisha huduma ya mama inaboreshwa baada ya kujifungua Shirika la So They Can Tanzania (STC), limeweka mitambo ya umeme wa nguvu ya jua katika Kituo cha Afya cha Mamire kilichoko Halmashauri ya Babati.

Meneja miradi wa shirika hilo, Godfrey Mogusu, alisema pia wamekabidhi vifaa vya kuchemshia maji ya moto ili kuwasaidia wanawake wanaojifungua na wakakosa huduma ya maji ya moto ya kufanyia usafi.

"Wafadhili hawa waliamua kuleta sola kituo hiki cha afya Mamire, kwa kuwa tulipokwenda nao kupanda Mlima Kilimanjaro, baada ya kurudi tukawaleta hapa nao waliwauliza wanawake wana shida gani wakaambiwa wanapomaliza kujifungua wanakosa maji ya moto ya kufanyia usafi, hivyo, ndio maana wameamua kuwasaidia," alisema Mogusu.

Aidha, alisema sola waliyoweka ina uwezo wa kuchemsha maji moja kwa moja na ina gharama ya Sh. milioni tano na vifaa ambavyo vitafungwa kwa ajili ya kusaidia kuchemsha maji vina gharama ya Sh. milioni nne.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Terri Anderson, akikabidhi sola hiyo na vifaa hivyo kwa wananchi, viongozi wa kituo hicho na viongozi wa halmashauri katika kituo hicho cha afya Mamire juzi.

Alisema msaada huo umetolewa na Chuo Kikuu cha Notre Dame cha Marekani kwa kushirikiana na Carren Colman wa nchini Australia.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamisi Malinga, alitumia fursa hiyo kuwashukuru So They Can kwa msaada huo ambao utasaidia kuweka umeme wa sola katika jengo la mama na mtoto ambalo lilikuwa halina umeme.

Mganga Mkuu wa kituo hicho, Dk. Fuatael Sossiya, aliwashukuru wahisani hao kwa kutoa msaada huo wa huduma ya upatikanaji wa maji ya moto ambao anasema utawasaidia wanawake wanaokuja kujifungua, huku akisema kituo hicho kinapokea wanawake wa kujifungua 15 kwa mwezi na kinahudumia watu zaidi ya 6,000 kwa mwaka.

## Madiwani wachachamaa wanafunzi waliochelewa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, limeihoji Idara ya Elimu Sekondari kuhusu hatua waliyoichukua ya kuwafuta wanafunzi 49 wasiojulikana sehemu walipo ambao waliotakiwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2018.

Wakizungumza kwa niaba ya madiwani wengine katika kikao cha kawaida cha baraza hilo cha robo ya pili ya mwaka, Diwani wa Kata ya Kiutu, Zephania Sirikwa, Lazaro Orasi Rasi (Kata ya Bwawani), na Elisante Nassari (Oldonyowasi), waliihoji Idara ya Elimu Sekondari kwa nini wachukue hatua ya kuwafuta wanafunzi hao bila ya kujua wanakabiliwa na tatizo gani.

Nassari, alisema kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi, kila mtu ana haki ya kwenda shuleni kupata elimu, hivyo, kufutwa kwa wanafunzi hao, kunawanyima kupata haki yao ya kimsingi.

"Katika kufuatilia, nilibaini kati ya wanafunzi 49, mmoja anatoka kata yangu na nilipomhoji aliniambia mama yake alikuwa anaumwa na alilazwa hospitali, ndiyo maana, alishindwa kuripoti shuleni mapema," alisema.

Aliongeza sababu iliyosababisha mwanafunzi huyo, kuacha shule alikuwa ndio mlezi mkuu wa familia baada ya mzazi wake kuwa mgonjwa na alikuwa anakabiliwa na changamoto ya ugumu wa maisha.

"Baada ya kuzungumza na mtoto aliniambia yupo tayari kurudi shuleni, mwenyekiti, mwanafunzi huyu tutamsaidiaje sababu hali ya maisha ndiyo ilimfanya kuacha shule na tayari wameshafutwa," alisema.

Sirikwa aliongeza kufutwa kwa wanafunzi hao, imelisababishia taifa kupoteza wataalamu wengi wa baadaye ambao wangeisaidia nchi kusonga mbele kimaendeleo.

Ofisa Elimu Sekondari kwenye Halmashauri ya Arusha, Sophia Msofe, alisema wanafunzi walichaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza kwa awamu ya kwanza walikuwa 248. Aidha, alisema baada ya ufuatiliaji walibaini wanafunzi 196 walikwenda shule za watu binafsi na wengine 49 hawakujulikana walipokuwa.

Aliongeza wanafunzi wataorudi na wapo tayari kuendelea na masomo ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Elimu Mkoa iko tayari kufanya utaratibu waendelee na masomo.

# Sheria ya uwekezaji EPZA sasa kufumuliwa

**Na Mary Mosha,** SIHA

SERIKALI imesema inataka kuifumua Sheria ya Uwekezaji ya Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA), ili kuondoa mkanganyiko uliopo wa tozo na kodi mbalimbali zinazotozwa na halmashauri na wakati huo huo kutozwa na mamlaka husika.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, ndiye aliyetangaza kusudio hilo jana, baada ya kufanya ukaguzi katika shamba la uzalishaji wa parachichi la kampuni ya kimataifa ya Africado iliyoko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

"Hivi sasa tuko katika mchakato wa maandalizi ya kupeleka Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya EPZA kwa ajili ya kufanya amendments (marekebisho) ili kuondoa hii mikanganyiko na malalamiko ya tozo na kodi zinazotozwa na halmashauri na EPZA. Kimsingi, jambo hili linachangia sana kutoelewana kati ya halmashauri na wawekezaji," alisema Kakunda. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, inatoa mamlaka kwa mwekezaji kusamehewa kodi kwa miaka 10.

Kakunda alikiri kwamba kwa sasa sheria hiyo imekuwa ikileta mkanganyiko baina ya wawekezaji na serikali katika ulipaji wa kodi.

Akiwa katika shamba hilo, Waziri Kakunda alipokea changamoto kutoka kwa Meneja Utawala wa Shamba la Africado, Paschal Shayo, juu ya mkanganyiko uliopo wa sheria ya ulipaji wa kodi kati ya halmashauri na EPZA.

Mwaka juzi, Africado waliuza kwa wingi parachichi katika masoko ya Ulaya, matunda zaidi ya tani 2,580.

Africado inauza kwa wingi parachichi inayolimwa Mkoa wa Kilimanjaro kwenye masoko ya Ufaransa, Denmark, Uholanzi na Sainsburys Waitrose ya Uingereza.

Parachichi kutoka Kilimanjaro ambalo linauzwa katika masoko hayo ni bora zaidi na linauzika zaidi kuliko lile linalochukuliwa katika masoko ya nchi ya Afrika Kusini na Peruvian.

Pia, parachichi linalozalishwa katika Mkoa wa Kilimanjaro linalifuta kwa kasi sokoni tunda kama hilo linalozalishwa nchini Israel.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika kijiji cha Lwezera wilayani Geita, ambacho kimepata umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini wa awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (REA III) juzi. **PICHA: WN**

# DC aagiza wanafunzi 500 kujifunza Kinapa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, ameagiza wanafunzi 500 wa kidato cha tano na sita kutoka mikoa mbalimbali nchini ambao wanachukua masomo ya Sayansi na hawajawahi kuona uoto wa asili wala miamba, wapelekwe katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro kujifunza kwa vitendo.

Buswelu amesema mbinu hiyo, itasaidia pia kuutangaza utalii wa ndani kwa kutumia wanafunzi, badala ya kutegemea watu maarufu na wasomi kuvutia wazawa kutembelea na kujionea vivutio na maajabu ya dunia.

"Wilaya yetu ina shule za sekondari sita zinazofundisha wanafunzi wa kidato cha tano na sita na wengi wametokea mikoa mbalimbali nchini. "Wengi hawajui uoto wa asili ukoje, jiolojia ni nini kivitendo? Kwa hiyo nimesema hii ni fursa nzuri kwao ya kujionea kwa macho aina ya vitu ambavyo wamekuwa wakifundishwa darasani kwa nadharia. Tunataka kuwaandaa wataalamu mahiri wa baadaye katika nyanja mbalimbali," alisema.

Kwa mujibu wa Buswelu, serikali ya wilaya hiyo imebuni mbinu ya kutangaza utalii wa ndani kwa kuwatumia wanafunzi wanaosoma katika wilaya hiyo kutokana na wengi wao kutokea katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ambayo haijawahi kuona uoto wa asili na mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika.

Kabla ya Buswelu kuja na wazo hilo, hivi karibuni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameitaka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), kuwatumia wasomi na watu maarufu kutangaza utalii wa ndani.

Shule za sekondari zilizoagizwa kupeleka wanafunzi hao ni Sanya Juu, Oshara, Magnificant, Visitation Girls, Magadini na Faraja Seminari.

Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ina vivutio lukuki ikiwamo mti mrefu kuliko yote barani Afrika, vilele vitatu virefu vilivyosimama, maporomoko ya maji, mimea iliyoota kwa mpangilio maalumu kadri navyokwea mlima huo na ndege wa ajabu wanaoishi katika maeneo baridi.

Mti huo aina ya mkukusu wenye urefu wa mita 81.5 na wenye umri wa zaidi ya miaka 600, uligunduliwa na watafiti wawili wa Chuo Kikuu cha Bayreuth cha Ujerumani, akiwamo Dk. Andreas Hemp, baada ya kufanya utafiti kwa miaka 31.

## Uchumi watishia ukuaji vijiji vitatu

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

HALI mbaya ya kiuchumi inayotishia kasi ya ukuaji wa vijiji vitatu vya Kibaoni, Nayeme na Nanjara vilivyopo katika Wilaya ya Rombo, imeelezwa kuwa inasababishwa na kukosekana kwa huduma ya maji kwa miongo kadhaa sasa.

Hivyo ni miongoni mwa vijiji ambavyo vinakabiliwa na tatizo kubwa la kukosa maji, ingawa pia nyakati za kiangazi, Wilaya ya Rombo huathiriwa zaidi na uhaba wa maji kutokana na kupungua kwa ujazo kutoka mita za ujazo 27,000 hadi kufikia 18,000.

Katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo, Meneja wa Kampuni ya Maji ya Kili Water ambayo inatoa huduma wilayani humo, Prosper Kessy, amesema tayari wamevitengea vijiji hivyo kiasi cha Sh. milioni 155 kuvipelekea huduma ya majisafi mwaka huu.

"Mradi huo utahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha maji kutoka msitu wa serikali wa shamba la Rongai, lenye urefu wa zaidi ya kilometa 12 na kuyasafirisha hadi tangi lililopo Kijiji cha Kibaoni, tayari kwa kusambaza katika vijiji vingine viwili vya Nayeme na Nanjara," alisema.

Januari 31 mwaka huu, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018, ambao pamoja na mambo mengine utaruhusu kuundwa kwa Wakala wa Maji Vijiji. Alisema mahitaji ya maji wilayani humo ni mita za ujazo zaidi ya 40,000, lakini upatikanaji wa maji ni mita za ujazo 27,000.

Akitetea hoja yake kuhusu tatizo la maji kutofika maeneo yote ya wilaya hiyo, Kessy alieleza kwamba tatizo linalochangia kukua kwa hali hiyo ni kuwapo kwa vyanzo vichache vya maji na ambayo vingi kati yake, hukauka mara kwa mara.

Alisema zaidi ya wakazi 20,700 wanapata huduma ya maji wilayani humo baada ya kuboresha huduma za upatikanaji wa maji. Awali kampuni hiyo wakati inaingia Wilaya ya Rombo kuanza kutoa huduma mwaka 1995, walikuta wananchi 5,200 wa majumbani, ndio walikuwa wameunganishiwa huduma ya maji.

Kili Water ilikuta mtandao wa usambazi maji, ulikuwa kilometa 700, lakini sasa umeongezeka hadi kufikia 1,200, huku vyanzo vya maji vikiongezeka kutoka vyanzo 24 hadi 30.

ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI FEBRUARI 21, 2019



Ukurasa 16

**Kila mzee Kahama sasa anafaidika kwa tiba bure kupitia bima ya afya**




Ukurasa 18

Matibabu moyo rasmi Hospitali Benjamin Mkapa



Ukurasa 14

**Mahakama: Ruksa kuendesha gari umekunywa**



# Kijue kinachogharimu wazazi wanaonyonyesha 'vichanga'

Ukurasa 19

## Mahakama: Ruksa kuendesha gari umekunywa

**Nairobi,** Kenya

MAHAKAMA ya Kiambu nchini hapa, imetoa uamuzi wa kipekee, ikisema uendeshaji gari baada ya kunywa pombe sio makosa, iwapo dereva analidhibiti gari.

Hakimu, Bryan Khaemba, amemtaja mshtakiwa dereva, Michael Mugo, aliyetuhumiwa kuendesha gari kwa ushawishi wa pombe hana kosa, kwani hakukuwepo ushahidi wa ulevi uliokwaza udereva wake.

Dereva huyo alishtakiwa kwa kuendesha gari akiwa mlevi hivyo, hakuwa na udhibiti mzuri wa gari lake. Askari wa Usalama Barabarani aliyetoa ushahidi katika kesi hiyo, alidai katika harakati za kumkamata dereva, alimshinda nguvu yeye na wenzake wawili, akawaponyoka.

"Hilo haliwezekani kwa mtu ambaye anadaiwa kuwa mlevi chakari," ilinukuu sehemu ya hukumu hiyo, ikimtetea mshtakiwa hakuathiriwa na pombe, kwani ana ushahidi wa kuwazidi nguvu polisi wa usalama barabarani.

"Naamuru kwamba upande wa mashtaka ulishindwa kuwakilisha kesi yenye ushahidi mzuri dhidi ya mshukiwa, kwa kushindwa kutoa ushahidi kwamba alishindwa kulidhibiti gari alilokuwa akiendesha,' alitamka hakimu.

Hukumu hiyo ilisisitiza kwamba, kuendesha gari kama mtu hajaathirika na pombe sio makosa.



Polisi wa Usalama Barabarani, jijini Nairobi, wakimkamata dereva. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

JPM ALIPOZINDUA

# Mradi wa maji unaonusuru meno kuoza, miguu na migongo kupinda

• Wakazi washangilia, wengine hoi majumbani

**Na John Ngunge,** ARUSHA

ZAIDI ya wakazi 40,000 wanaoishi Kata za Oldonyosambu, Oldonyowas na Engikareti wilayani Arumeru, ambao tangu uhuru wameteseka utumia maji yanayoelezwa kuwa na kiasi kikubwa cha madini ya 'fluoride'baadhi kudaiwa kudhurika kwa namna tofauti kama kupinda miguu na migongo, kumeizindua serikali kuchukua hatua ya kuwanusuru watu hao.

Sasa Rais Dk. John Magufuli, ametaka utekelezaji wa mradi mkubwa wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha, (AUWSA), aliyoweka jiwe la msingi mnamo Desemba 2, mwaka jana kupeleka maji kwa wakazi wa Oldonyosambu.

Ingawa eneo la Oldonyosambu halipo chini ya utekelezaji wa AUWSA, lakini kupitia agizo la Rais Dk. Magufuli, Wizara ya Maji, inalazimika kutafuta fedha za kusambaza mabomba ya maji kutoka chanzo cha maji kilichopo Kimnyak, wilayani Arumeru, kwenda hadi Oldonyosambu.

Mbali na dai la kupinda migongo na miguu, baadhi ya watoto wanaozaliwa na kutumia maji hayo wanapata madhara ya kuwa vichwa vikubwa na kudumaa mwili.

Eneo hilo linakadiriwa kuwa na madini ya fluoride yenye kiasi cha miligramu 19 hadi 20 kwa lita moja ya maji, kiasi kinachoelezwa ni kikubwa na kinachosababisha madhara kwa matumizi ya kunywa na kupikia.

Kiwango kizuri cha fluoride kilichopendekezwa na Shirika la Afya Duniani, (WHO), ni 0.5 miligramu kwa lita moja ya maji.

Wataalamu wanasema 'fluoride' ni madini yenye madhara makubwa kwenye mifupa, uti wa mgongo, meno kuwa kahawia na kuyafanya yasiwe magumu, hivyo yanashambuliwa kirahisi na bakteria na kuathiri mfumo wa ukuaji ubongo, hasa watoto kushindwa kukomaa vizuri.



Rais Dk. John Magufuli, akizungumza na wakazi wa Oldonyosambu, wilayani Arumeru. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

> **Kuna watoto miguu imejikunja (pinda), mingine inaonekana kama pasi na wanakuwa na vichwa vikubwa.**



Mkazi wa Odonyosambu, Mkoa wa Arusha aliyeathiriwa meno na maji.

**DK. CHANDE**

Msimamizi wa Kitengo cha Huduma ya Kinywa na Meno, Dk. Omary Chande, ambaye ni Msaidizi wa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa, anasema, watu wanaokunywa maji yenye madini mengi ya 'fluoride' wanapata athari ya kupinda mifupa, meno kubadilika rangi au wengine meno yao yanasagika.

Dk. Chande anasema ni magonjwa yasiyo na tiba kwa wagonjwa wa aina hiyo, kwa sababu ni ngumu kutoa mifupa iliyopinda, isipokuwa msaada kwa magonjwa yanayoambatana nayo.

**WAKAZI**

Mkazi wa Kijiji cha Lamanda, Arumeru, Doro Stephen Mollel (56), anasema maji wanayotumia wakazi wengi kijijini hapo yana madhara makubwa kwa watu wazima, wajawazito na watoto.

"Yanawaathiri kwa sehemu kubwa, kwanza mjamzito anapokunywa hayo maji yanaenda kumathiri mtoto ambaye bado hajazaliwa.

"Anapojifungua sehemu kubwa ya muda huo anatumia maji hayo kwa wingi zaidi na hivyo kuathiri mtoto makuzi ya mtoto...madhara yake yanaonekana mtoto anapoanza kutambaa, anashindwa kwa kuwa viungo vyake vinakuwa legelege na vimedumaa.

"Viungo vinavyoonyesha ulemavu kwa mtoto, ni kichwa chake kuvimba na kuwa kikubwa tofauti na maumbile yake wakati wa kuzaliwa.

"Pia, fluoride inaifanya mifupa ya watoto kuwa legelege na miguu kupinda," anasema na kuongeza, kwa watu wazima inawafanya waonekane wamezeeka mapema kabla ya umri wao.

Mollel anasema, wakazi wengi katika kijiji hicho hususani wanaotoka ukanda wa chini barabara inayoelekea Namanga kutoka Arusha mjini, wamepinda migogo na miguu, kwa sababu ya kutumia maji yenye fluoride nyingi, ilhali hawana maji mbadala.

Anasema eneo la ukanda wa juu, yaani, upande wa kulia wa barabara hiyo hali ni nafuu zaidi kwa kuwa wakazi hao wamefanikiwa kupata chanzo kidogo cha maji yasiyo na madini hayo kutoka eneo la Shambasha jirani na Msitu wa Hifadhi uliopo Mlima Meru.

Mollel anasema juhudi zao

AFYA

# Mradi wa maji unaonusuru meno kuoza, miguu na migongo kupinda

wameweza kusambaza maji hayo katika maeneo kadhaa na wengi wameanza kuyatumia.

Anasema binafsi akitokea ukanda huo husika, amekumbwa na matatizo ya kuumwa mgongo kila mara, aliamua kujiwekea utaratibu wa kufuata maji ya bomba eneo analolitambulisha kuwa ni madukani, kwa ajili ya matumizi ya kunywa na kupikia tu.

"Ninakuja kuchota maji hapa madukani na kutembea na dumu kichwani umbali wa kilomita sita hadi nyumbani kwangu. Wakati mwingine huwa napata usafiri wa magari ya abiria hivyo naweza kuchukua madumu mawili ya maji ya lita 20 kila moja," anasema.

Matumizi mengine kama vile kufua nguo, huwa anatumia maji ya fluoride yanayopatikana kwenye visima.

"Naogopa kutumia maji haya, yalinitesa sana kwa kuumwa mgongo mara kwa mara, hivyo niliamua kuacha kuyatumia kwa kunywa au kupikia wakati nikiwa na mtoto wa tatu," anasema Doro ambaye ni mzazi wa watoto sita.

"Hata watoto wangu wakiwa shule ninawawekea maji salama kwenye chupa kwa ajili ya matumizi yao au ninawataka kunywa maji salama ya bomba...sasa si unajua tena watoto, wakati mwingine huwa wanatumia tu maji ambayo siyo salama," anasema.

Mwenyeji mwingine, Flora Mollel, (60), anasema, tatizo la madini ya fluoride limeathiri sana jamii ya Kimasai inayozunguka maeneo hayo.

"Wapo wenzetu walioathirika kiasi cha kushindwa kutembea. Wanalazimika kutuma madumu kama msaada wa nguzo ya kutembea na kuingia ndani ya maboma yao.

"Waathirika wa tatizo hili ni wengi, lakini wanafichwa hasa wale ambao hawawezi kutembea kwa nguvu zao bila msaada. Hawatoki tena....haya maboma yana siri nyingi eti.

"Yaani baba, hata wengine ukiwaona tu unaona uchungu kwa jinsi wanavyoteseka. Haya maji yaliyopo ukanda huu wa chini wa Lemanda, hayafai kabisa kwa matumizi.

"Kuna watoto miguu imejikunja (pinda), mingine inaonekana kama pasi na wanakuwa na vichwa vikubwa," anaeleza.

Anasema awali walidhani tatizo hilo linasababishwa na ukosefu wa lishe na hiyo ilisababisha wataalamu wa lishe waliofika kwao na wakafundisha.

Hata hivyo, anasema iligundulika baadaye kwamba tatizo halikuwa lishe, bali ni maji yenye kiasi kikubwa cha madini ya 'fluoride.'

Anasema, binafsi alishapata madhara ya ugonjwa huo, baada ya kujifungua mtoto wa tatu mwaka 1986, kwani kabla ya kumaliza mwezi, alijisikia maumivu makali kwenye uti wa mgongo.

"Ukisikia maumivu kama hayo, lazima mgongo upinde, maumivu yanapitia uti wa mgongo. Nilipelekwa kwa matibabu Hospitali ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, ambako nililazwa kwa muda wa miezi mitatu nikiwa natumia kitanda cha mbao kuunyoosha mgongo," anasema.





Watoto wa Odonyosambu, Mkoa wa Arusha, walioathirika miguu kutokana na maji kuwa na athari ya madini.

> "Yaani baba, hata wengine ukiwaona tu unaona uchungu kwa jinsi wanavyoteseka. Haya maji yaliyopo ukanda huu wa chini wa Lemanda, hayafai kabisa kwa matumizi.

**NURU YA RAIS**

Mara tu baada ya Rais Dk. John Magufuli, kuweka jiwe la msingi la mradi wa AUWSA, hafla katika halfa iliyofanyika katika kijiji cha Kimnyak, wilayani Arumeru, wakazi wanaona mwanga kwa ufumbuzi wa tatizo hilo.

Mradi huo unaofadhiliwa kwa mkopo wa Shilingi bilioni 520 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), utakapokamilika utatoa lita milioni 208 za maji kwa siku, hivyo kumaliza tatizo la maji kwa wakazi wa jiji la Arusha na vijiji saba, ambavyo bomba la maji litapita. Mahitaji ya maji kwa wakazi wa jiji la Arusha, ni lita milioni 94 kwa siku.

Katika hafla hiyo ya kuweka jiwe la msingi, Rais Magufuli, aliagiza mradi huo kupeleka maji ya bomba katika maeneo ya vijiji vya Oldonyosambu, ambavyo vinakabiliwa na tatizo la maji kiasi cha wakazi kutumia maji yenye kiasi kikubwa cha madini ya 'fluoride.'

Wizara ya Maji na Umwagiliaji, hivi sasa ina jukumu la kutafuta fedha za kutandaza mabomba hadi Oldonyosambu, ili kutekeleza ahadi ya Rais Dk. Magufuli kwa wakazi hao.

Kabla ya kutekelezwa hatua hiyo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kushirikiana kampuni ya O2 and B imetoa mtambo maalum 'Capacity of Dionization System' (CDI), kupunguza kiwango cha madini ya fluoride kilichozidi kwenye maji yanayotumiwa na wananchi wa kijiji cha Lemanda.

Mtambo huo uliotolewa mwishoni mwa Desemba mwaka jana, umefanyiwa majaribio na watalamu wa kampuni hiyo kutoka China ambao ndio watengenezaji wakuu wa mitambo hiyo na tayari umesimikwa kijiji hapo kwa kuanza kazi.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Dk. Wilson Mahera, anasema wamepokea mtambo huo kutoka serikali kuu kupitia Wizara ya Maji.

Mtambo huo una uwezo wa kuchuja maji kwa kiwango kikubwa na kupunguza kasi ya madini ya fluoride kwenye maji.

"Mtambo huu una uwezo mkubwa wa kupunguza kiwango cha madini hayo kilichozidi pamoja na chumvichumvi kwenye maji, kwa kutumia teknolojia hii ya kisasa ya kuchuja maji bila kutumia kemikali kitapunguza madhara kwa wananchi wetu," anasema.

Mtambo huo una uwezo wa kuchuja maji na kupunguza kiwango chafluoride kutoka miligramu 18.7 kwa lita moja hadi kufikia miligramu 0.37 kwa lita moja.

"Matarajio ya serikali ni kukabiliana na tatizo hili na litamalizika na kutoa matumaini mapya kwa wananchi wa Lemanda kutooza meno na kupinda miguu kutokana na matumizi ya maji yenye madini ya fluoride," anasema.

Mapema kabla ya kuletwa mtambo huo, Halmashauri ya Arusha iligawa seti 80 za ndoo maarufu kama tanki za kuchujia, maji ya kunywa kwa kaya 80 za kijiji cha Lemanda, kwa lengo la kupunguza sumu ya madini hayo za wastani wa watu sita mpaka nane, kwa kila kaya.

Dk. Mahera amewataka wakazi hao kuhakikisha wanachuja maji ya kunywa na kupikia, ili kupunguza madini hayo na zaidi kupunguza athari zake kwa binadamu.

Halmashauri hiyo imeahidi kuendelea kununua seti hizo za ndoo kwa wakazi walioathirika zaidi, wakati ikiandaa mipango ya kudumu kutatua tatizo hilo kwa wakazi wa Oldonyosambu.

**SERIKALI MTAA**

Diwani wa Kata ya Oldonyosambu, Raymond Larumbe, anaeleza furaha yake kwamba kilio chao cha miaka mingi, cha wananchi hao hatimaye kimefikia serikalini.

Anasema, wananchi hao wamepata madhara makubwa, kutokana na matumizi ya maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya fluoride, huku watoto wadogo wakiathirika zaidi kwenye mifupa kwa kupinda miguu na kuwa na vichwa vikubwa.

"Nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kuokoa uhai wa wananchi wa Lemanda na kwa hili serikali imeonyesha njia ya kuwajali watu wake bila kuangalia itikadi za kisiasa," anasema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Gaspar Mollel, anauona mtambo huo, kwamba ni neema kwa wananchi wa eneo hilo, kwa sababu wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji maji safi na salama kwa matumizi ya majumbani.

Msimamizi Mkuu wa Maabara ya Ubora wa Maji Mkoa wa Arusha, Jovitus Kichumu, anasema kiwango cha madini ya fluoride kwenye maji yanayopatikana Kijiji cha Lemanda, Oldonyosambu ni miligramu 18.7 kwa lita moja, kiwango ambacho kikubwa na kisichofaa kwa matumizi ya binadamu.

AFYA

# Kila mzee Kahama sasa anafaidika kwa tiba bure kupitia bima ya afya

**Na Marco Maduhu,** Kahama

KATIKA sehemu nyingi nchini kuna vilio vya kudai haki ya usalama na tiba kwa wazee, ambayo iko kisheria.

Ni kauli inayoanza kwa jamii iliko hadi mamlaka za juu za kiserikali, zikitaka hatua zichukuliwe katika hilo, kupitia halmashauri nyingi.

Moja ya maeneo hayo ni katika Halmashauri ya Mji Kahama, ambako kuna jumla ya wazee 10,232 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012; wanawake wakiwa 5,477 na wanaume 4,556.

Wazee hao ni wenye umri kuanzia miaka 60 na kati yao, asilimia 96 wako katika mazingira magumu ya maisha, kutokana na hapo awali hawakuwa na shuguli bora za kiuchumi au ajira asilimia nne pekee, ndio waliokuwa na ajira na kupata mafao ya kuwainua kiuchumi.

Kutokana na kundi hilo la asilimia 96 kukabiliwa na ugumu huo wa maisha, wamekuwa wakikosa hata fedha za kukidhi maisha yao ya kila siku.

Ikirejewa mantiki ya kawaida, ni kwamba hata mtu anapofikisha umri wa kuitwa mzee, inakuwa na maana hana nguvu tena ya kufanya kazi ya kumuingizia kipato, maisha yake kwa asilimia 99 yanabaki kulelewa na watoto wake.

Imebainika kwamba, kuna sehemu kubwa ya wazee hao wametelekezwa na watoto wao, na hasa wanaoishi vijijini baadhi wakiwa wanawalea wajukuu, hali inayowaweka katika ugumu wa maisha na hata kuwageuza wajukuu hao vitega uchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Vita Kawawa (katikati), akionyesha kwa vitendo, bango inapotakiwa kuwekwa kuhusu tiba ya wazee hospitalini. Kushoto, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu na kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kahama, Anderson Msumba. **PICHA: MTANDAO.**

### BAJETI YA WAZEE

Kutokana na mustakabali huo, Halmashauri ya Mji Kahama, imeamua kutenga bajeti ya wazee kwa kila mwaka wa fedha, ili kuwakatia bima ya afya ya jamii (CHF), itakayowaboreshea huduma za bure za matibabu.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa halmashauri hiyo, Abrahiman Nuru, anasema katika mwaka wa fedha uliopo 2018/19 walitenga Shilingi milioni 10 za kuwakatia wazee 6,247 kadi za Bima ya Afya ya CHF iliyoboreshwa, kwa kila mmoja.

Anasema kwa mwaka wa fedha ujao, 2019-20, watatenga kiasi cha Shilingi milioni 11, kwa ajili ya kuwakatia wazee wapatao 2,340.

"Baada ya kupokea changamoto hizi za ukosefu wa fedha za matibabu kwa wazee kutoka kwenye Shirika la Tawlae ambalo linatetea haki za wazee, halmashauri yetu ndipo ikaona umuhimu wa kuwatengea bajeti ya fedha kutoka kwenye mapato ya ndani, ili kuwatatulia tatizo hili la ukosefu wa matibabu bure," anasema Nuru.

"Mbali na fedha hizo kuwakatia bima hiyo ya afya, pia zimekuwa zikitumika kwenye masuala yao mbalimbali ikiwamo maadhimisho ya siku ya wazee duniani, vikao vyao na kuwapatia kadi za matibabu bure, wale wazee ambao bado hawajapata kadi za bima ya afya - CHF wakati akisubiri bajeti ijayo," anaongeza.

**"Tumekuwa tukitekeleza miradi mingi inayohusu wazee mkoani Shinyanga, ikiwamo ya kutokomeza mauaji dhidi yao, kutokana na imani potofu za kishirikina.**


Katibu wa Shirika la Tawlae, linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, Hellena Maleza, akielezea changamoto wanazokutana nazo wazee, wanapohitaji matibabu.

Nuru anasema ukataji bima hiyo itakuwa endelevu, ambapo na kinachofanyika sasa ni kuendelea kubaini wazee wapya waliokwishafikisha umri wa miaka 60 na zaidi, ili waingizwe kwenye bajeti hiyo ya bima ya afya.

### MWENYEKITI WA WAZEE

Wilfred Bilago, Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Halmashauri ya Mji Kahama, anaipongeza halmashauri kuwatengea bajeti inayowanufaisha na huduma ya bima ya afya iliyoboreshwa.

"Idadi kubwa ya wazee wamekuwa wakipoteza maisha, kwa sababu ya ukosefu wa fedha za matibabu, kutokana na ufukara wa maisha, sababu ya kumaliza nguvu za kufanya kazi ya uzalishaji mali, huku wengine wakitelekezwa na watoto wao, hatimaye kudhofika afya na kufariki dunia," anasema Bilago.

"Mtu anapokuwa na umri wa miaka 60 na kuitwa mzee, kinga zake za mwili zinakuwa tayari zimeanza kuchoka na matokeo yake, huanza kuandamwa na magonjwa mbalimbali kila kukicha, ikiwamo moyo, figo, sukari, presha na kibofu cha mkojo. Tiba zote hizi zinahitaji pesa na kama hauna kifo kinakuita,"anaongeza.

Anderson Lyimo, ni Katibu wa Baraza la Wazee Halmashauri ya Mji Kahama, anasema ukataji bima ya afya CHF, ni vyema ikatengewa madirisha kwenye vituo vya kutoa huduma za afya, ikiwamo na Hospitali ya Wilaya Kahama, ili kuwaboreshea huduma zaidi.

Anasema, pindi wazee wanapofuata matibabu kwenye maeneo ya huduma, hukutana na vibao vya 'wazee kwanza,' lakini hakuna madirisha yao, hivyo inapotokea wanawapita wagonjwa wengine wanakasirikia, kitendo kinachobeba sura ya kero zaidi kwao.

"Tunaipongeza Halmashauri ya Mji Kahama, kwa kutujali sisi wazee, lakini kuna kero ndogo ambazo zinahitaji kutatuliwa, ikiwamo kutengwa madirisha ya wazee, upatikanaji dawa kwa wingi zinaohusu tiba za wazee, pamoja na kutuwekea madaktari wetu," anaeleza Mzee Lyimo.

### WADAU HUSIKA

Mwenyekiti wa Bodi wa Huduma za Afya Halmashuari ya Mji Kahama, Dikson Maganga, anakiri kuwepo changamoto hizo, akiwa miongoni mwa waliokwisha kukutana na kadhia hiyo, alipothubutu kuwapita wagonjwa kwenye matibabu.

"Hii ni changamoto kubwa sana ya ukosefu wa madirisha ya wazee kwenye huduma zetu za kiafya, ikiwamo hospitali yetu ya wilaya, jambo nimelichukua na nitakwenda kuliwasilisha kwenye vikao vyetu, ili lipate kufanyiwa kazi," anasema Maganga.


Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Halmashauri ya Mji Kahama, Wilfred Bilago (wa kwanza kushoto), akiwa na katibu wake, Anderson Lyimo, kwenye kikao cha Shirika la Tawlae la kutetea haki za wazee mkoani Shinyanga.

Eliasenya Nnko, ni Mratibu wa shirika la Tawlae, linaloshughulikia utetezi wa haki za wazee mkoani Shinyanga, anasema katika utekelezaji wa miradi yao na changamoto ya wazee kuishi maisha magumu.

**"Tulipokuwa tukitoa elimu kwa wananchi kuacha mauaji hayo, ndipo tukakutana na changamoto hii ya wazee wengi kuishi maisha magumu.**

Anasema, kuna idadi kubwa ya wazee waliopoteza maisha kwa sababu ya ukosefu wa fedha za matibabu, ndipo walipoanzisha mradi mwingine unaoifanya mifumo ya utawala kuwajibika kwa wazee, ikiwamo halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya wazee.

"Tumekuwa tukitekeleza miradi mingi inayohusu wazee mkoani Shinyanga, ikiwamo ya kutokomeza mauaji dhidi yao, kutokana na imani potofu za kishirikina.

"Tulipokuwa tukitoa elimu kwa wananchi kuacha mauaji hayo, ndipo tukakutana na changamoto hii ya wazee wengi kuishi maisha magumu," anabainisha Nnko.

"Baada ya kuona hili ni tatizo, ndipo tukapata wazo la kuanzisha mradi mwingine wa kuishawishi mifumo ya utawala, zikiwamo halmashauri kutenga bajeti za fedha kwa ajili ya kutatua changamoto hizi za wazee, ikiwamo kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure, ili kuokoa afya zao," anaongeza.

Anataja matunda ya mradi katika halmashauri hiyo ni kwamba,.imeenda mbali zaidi ya kutoa vitambulisho hivyo vya matibabu, sasa wazee wanapatiwa bima ya afya ya CHF, jambo analolitaja la kuigwa na halmashauri zote nchini kuwanusuru wazee waliko.

# Wafalme China walivyotumia kalenda, hesabu kutanua uzazi

IKIREJEWA historia kuanzia kupiga hesabu ya nyakati mpaka kuvuka bahari, hesabu ndio utaalamu ambao falme na ustaarabu wa watu wa kale waliutegemea.

Safari ya uvumbuzi wa hesabu ina mizizi mirefu. Historia inaeleza, ilianzia Misri, kisha Mesopotamia na Ugiriki, lakini baada ya dola hizo kuanguka, maendeleo ya hesabu nayo yalianguka.

Kwa upande wa Mashariki, mambo yalikuwa tofauti na hatua kubwa zilikuwa zikipigwa. Hesabu ndiyo ilikuwa kiungo tegemezi cha kusimamisha maajabu ya dunia mpaka sasa.

Namba, zina nafasi muhimu katika kupangilia maisha katika nyumba ya ufalme.

### HESABU ZILIVYO

Kalenda na mwenendo wa sayari ndio zilichangia maamuzi yote ya Mfalme, mfumo wote wa maisha yake, mchana na usiku, jinsi ilivyopangiliwa.

Washauri wa mfalme walitengeneza mfumo uliomuwezesha kukutana kimapenzi na idadi kubwa ya wanawake waliokuwa chini ya milki yake, mpangilio wa hisabati huo ukionyesha namna ambavyo wiki mbili tu, kwa maana ya siku 15, anakutana na wanawake 121.

Kupitia mpangilio huo wa kimahesabu, anakutana na Malkia; wapenzi wakuu watatu; wake wadogo 27; na watumwa 81.


Sanamu ya Mfalme wa Kale China. **PICHA: MTANDAO**

Kutokana na mfumo huo, wataalamu wa hesabu walimuwezesha mfalme kuwa na kalenda ambayo ilimfikia kila mwanamke aliyekuwa katika milki yake.

### NGUVU ZA MFALME

Si nyumba tu ya mfalme ndio ilitegemea hesabu hiyo, bali mambo yote ya utawala wa nchi.

Usiku wa kwanza ulitegwa maalumu kwa Malkia. Usiku wa pili kwa wapenzi wake wakuu watatu. Wake zake tisa walipewa usiku wa tatu, na baada ya hapo wake wadogo 27 walitumia usiku nao na Mfalme.

Baada ya hapo katika kipindi cha siku tisa zilizofuata, watumwa tisa tofauti walilala na mfalme kila siku.

Mfumo huo uliwekwa maalumu, ili wanawake wenye wadhifa mkubwa zaidi, watumie na Mfalme katika kipindi ambacho mwezi unaangaza zaidi, kipindi anachokuwa na nguvu zaidi za kimapenzi, ili zinazomudu kukabiliana na nguvu za Mfalme.

Kuwa mfalme, alihitajika mtu awe na nguvu za kutosha, lakini malengo yalikuwa wazi, kuzaa wana-mfalme wengi iwezekavyo, ili kuwezesha jami ya kifalme iendelee na itanuke.

Si nyumba ya mfalme tu ndio ambayo ilitegemea hesabu, bali mambo yote ya utawala wa nchi.

China ya kale ilikuwa na eneo kubwa ambalo lilitawaliwa kwa sheria kali, zikiwemo za kodi, vipimo vya uzani na pesa.

Ilikuwa na eneo kubwa lililotawaliwa kwa sheria kali, zikiwemo za kodi, vipimo vya uzani na pesa.

Dola hiyo ilitumia mfumo wa desimali miaka 1000 kabla ya nchi za Magharibi kuanza kutumia. Wachina walikuwa wana mifumo ya hisabati, ambayo haikuonekana katika nchi za Magharibi, hadi mwanzoni mwa karne ya 19.

Simulizi za kale zinaelezwa kuwa Mtawala wa Kwanza wa China, aitwaye Mfalme wa Njano, alitengezewa hisabati akiwa na moja ya Miungu yake mwaka 2800, kabla ya kuzaliwa Kristo, akiamini fani hiyo ina nguvu kubwa.

Mpaka sasa, Wachina wanaamini katika nguvu hizo za ajabu za nambari. Namba tasa zinachukuliwa kuwa ni za kiume na shufwa ni za kike.

Namba nne huepukwa na nguvu zote, wakati namba nane huleta bahati nzuri. **BBC**




AFYA

# Matibabu moyo rasmi Hospitali Benjamin Mkapa jijini Dodoma

- Maabara ya bil. 5/-; tiba nje yapungua 95%

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (aliyeko mbele) akizindua Maabara ya Uchunguzi na Tiba ya Magonjwa ya Moyo (Cath-lab), katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma. Kushoto, ni Katibu Mkuu wake, Dk. Zainab Chaula na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**




**Na Yasmine Protace**

HUDUMA za matibabu ya moyo, awali iliwagharimu wagonjwa kuzifuata nje mbali ya makazi yao na hata nje ya nchi, kwani zilipatikana kwa tabu nchini.

Mbali na kuzifuata nje ya nchi huduma hizo, serikali nayo ilitumia pesa nyingi kuwapeleka nje wagonjwa kutibiwa.

Sasa kuna mageuzi kwamba katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma, ambako kumeanzishwa huduma za matibabu ya moyo kwenye maabara ya uchunguzi na tiba ya magonjwa ya moyo, wakitumia mashine iitwayo 'Cath-lab.'

Maabara hiyo ya tatu nchini na ya pili kwenye taasisi ya serikali, inatarajiwa kutoa huduma za uchunguzi na tiba ya magonjwa ya moyo ndani ya muda mfupi, hivyo kuhudumia wagonjwa wengi ndani ya muda mfupi.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa maabara hiyo, mgeni rasmi Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy

> **Maabara hiyo ya tiba ya moyo, imegharimu kiasi cha Shilingi bilioni tano na inatarajiwa kuwa msaada mkubwa katika matibabu hayo.**

Mwalimu, anasema kufunguliwa maabara hiyo, ni mafanikio makubwa kwa serikali katika kusogeza huduma za kibingwa karibu na wananchi waliko.

"Huduma za kibingwa zimepunguza idadi ya wagonjwa waliokuwa wanasafiri au kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu kwa asilimia 95 kutokana na uboreshaji wa huduma za afya ndani ya nchi," anasema Waziri Ummy.

Anasema, serikali imekuwa ikiwajengea uwezo wataalamu wa afya nchini waweze kutoa huduma bora kwa wananchi, jambo ambalo limezaa matunda kwa wagonjwa wengi hivi sasa kupatiwa matibabu ndani ya nchi.

### RUFANI IKOJE?

Waziri Ummy anatoa ufafanuzi wa upatikanaji wa rufani ya matibabu nje ya nchi, kwamba serikali haijazuia, bali ni lazima kujiridhisha kwanza huduma za matibabu zinazotakiwa hazipatikani nchini, ndipo rufani inatolewa.

"Hakuna daktari tuliyemkataza kutoa rufani nje ya nchi. Sasa hivi tuna uwezo wa kutoa huduma za matibabu ya kibingwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lazima daktari awe amejiridhisha na kuthibitisha kwamba matibabu hayo hayapatikani nchini kabla ya kutoa rufani," anasema.

Waziri Ummy anaupongeza uongozi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa na Taasisi ya Jakaya Kikwete, ubunifu wao wa kushirikiana kutoa huduma bora za matibabu ya moyo, kwa wananchi na anazitaka hospitali na taasisi nyingine za afya, kuiga mifano yao katika uboreshaji huduma za afya nchini.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy anawataka wananchi kujiunga na Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya, ili waweze kupata bima ya afya itakayowasaidia kupata huduma za matibabu kwa uhakika.

Huku ikitangazwa mikakati ya kuwepo kwa raia wote nchini, waziri anahimiza umuhimu wake kwa Watanzania kuwa nayo, hali itakayowapunguzia gharama za matibabu.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, anasema ipo haja ya kuwathamini madaktari wazalendo, wanaojitoa kuokoa maisha ya wagonjwa, huku akiwahakikishia serikali itabaki imara kuwathamini.

Dk, Zainab anasema kuwa serikali itaendelea kuwekeza katika wataalamu wa afya nchini, ili adaktari bingwa wengi wanaotoa huduma za kibingwa hapa nchini, pamoja na kuwekeza kwenye miundombinu na vifaa.

### WATENDAJI AFYA

Pia, Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Mohammed Kambi, anatoa rai kwa wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha, kufanya mazoezi na kula chakula bora ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza, yakiwemo kisukari na shinikizo la damu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, anasema kuwa maabara hiyo ya tiba ya moyo, imegharimu kiasi cha Shilingi bilioni tano na inatarajiwa kuwa msaada mkubwa katika matibabu hayo.

Anasema, mafanikio katika huduma hizo za kiuchunguzi, zitasaidia kupunguza adha ya wagonjwa kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu, ambazo awali zilipatikana jijini Dar es Salaam, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na hospitali nyingine binafsi.

Dk. Chandika, anatoa kauli ya kuunga mkono, akisema wataendelea kushirikiana na wataalamu kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, ili kufanikisha uwepo wa jambo wanalonuia, mbalao ni kuwepo huduma bora kwa wananchi.

Pia, anataja fursa hiyo kuiomba serikali iongeze idadi ya wataalamu, ili kuboresha zaidi upatikanaji wa huduma za afya kwa umma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Profesa Mohamed Janabi, anasema kuwa hadi kufikia jioni ya siku hiyo, kuna wagonjwa 13 kutoka Dodoma na mikoa jirani walishawafanyia uchunguzi katika maabara hiyo ya Dodoma na kati yao, wanne walitakiwa kwenda JKCI kwa uchunguzi na tiba zaidi.

Profesa Janabi, anatumia nafasi hiyo kuishukuru Hospitali ya Benjamin Mkapa, kuwapa nafasi na heshima kushirikiana katika utoaji huduma za matibabu kwa wananchi.

AFYA

WIKI YA UNYONYESHAJI

# Kijue kinachogharimu wazazi wanaonyonyesha 'vichanga'

**Na Lilian Lugakingira**, Missenyi

• Azaliwaye aishia kupewa maji vuguvugu • Watosa ya kliniki, mila zinachukua nafasi • Uelewa 'sifuri' maziwa ya titi kukaa siku na nusu

MTOTO alitumwa mara kwa mara. Hakuongezeka uzito. Nilipokwenda kliniki nilitukanwa na wauguzi, lakini Mungu alimnusuru hadi sasa yuko hai anaendelea vizuri," anasimulia Farida Ishengoma, mkazi wa kijiji na kata ya Kilimilile, wilayani hapa, mkoa wa Kagera.

Mama huyo anarejea tatizo la wanawake wenzake kutowanyonyesha watoto maziwa yao ndani ya saa moja baada ya kujifungua, kwamba limekuwa likisababisha madhara ya kiafya kwa watoto, wageni duniani.

Inaelezwa kupitia taaluma ya afya, kwamba ni hali inayomfanya mtoto mgeni duniani ashindwe kutoa kinyesi cha kwanza na hivyo anapata homa za kila mara.

Kinachoelezwa ni kwamba kinamama hao wanashindwa kuwanyonyesha watoto maziwa, dai lao kuu ni kwamba maziwa hayo ya kwanza ni machafu, kutokana na rangi yake ya njano.

### MHUSIKA AJIELEZA

Mama Farida, anasema alipojifungua mtoto wa kwanza, alikuwa na mawazo hayo ya kutomnyonyesha 'kichanga' wake, badala yake alimpatia maji vuguvugu kwa maelekezo ya mwenzake aliyekuwa naye hospitalini.

Anakiri alichukua hatua hiyo, wakati alishaelezwa umuhimu wa maziwa hayo anapojifungua kwenye Kituo cha Afya Bunazi wilayani hapa.

"Nililazimisha kukamua na kuyaangalia. Niliona kama yana majimaji na rangi ya njano. Nikadhani bado ni machafu. Sikumnyonyesha kwa wakati huo, badala yake nilimnywesha maji ya vuguvugu," anaeleza.

"Baada ya muda kama wa saa mbili, nilichukua tena maji kumnywesha mtoto, maana nilikuwa sijaamini kama maziwa yamekwishakuwa safi.

"Lakini mama mmoja aliyekuwa amelazwa jirani yangu alinikemea, akanizuia nisimpe mtoto maji. Akinataka nimnyonyeshe badala ya kumnywesha maji," anasema.

Farida anasema, japo alifuata maelekezo ya mama yule wodini, alihisi woga na maumivu aliyodhani yanatokana na kumlazimisha mtoto kunyonya wakati matiti hayatoi maziwa ya kutosha.

"Niliendelea kumnyonyesha hivyo hivyo, lakini kesho yake nilihisi maziwa kama yameongezeka. Kwa hiyo, nikaendelea kumnyonyesha bila matatizo, lakini baadaye nikafanya kosa jingine la kumpa vyakula vya ziada kama chai na uji kabla ya kutimiza miezi sita," anasema.

Mama huyo anasema alifikia hatua hiyo katika kipindi cha kilimo au alipenda kufanya vibarua vya kujikimu. Alikuwa na utaratibu wa kuondoka akiwa ameacha tayari ameshachemsha ama chai au uji mwepesi, ili mtoto anapolia amnyweshwe bila ya kujua kama analolifanya ni kosa kwa afya ya mtoto.

Farida anasema afya ya mtoto ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 10, alipokuwa na umri chini ya mitano, aliugua kila mara na sababu kuu alibaini baadaye ni kutomnyonyesha maziwa ya mwanzo

Farida anakiri kubadilika kwa hivi sasa hawezi kufanya tena kosa la aina hiyo, kwani amekwishafahamu umuhimu wa kutompa mtoto vyakula vingine ndani ya miezi sita ya kuzaliwa.

Anasema, katika uzazi wa mtoto wake wa pili alifuata maelekezo aliyoyapata kutoka kwa wataalamu wa afya na hakuugua kama wa mwanzo.

Farida anakiri ni zao la mdogo wakati alipojifungua mtoto wa kwanza, huku akigusia upande wa pili wa baadhi ya kinamama walishakuwa na ufahamu bora juu ya umuhimu wa kumnyonyesha mtoto maziwa ya kwanza, ndani ya saa moja ya kujifungua.



Mama akimnyonyesha mwanawe.. **PICHA: MTANDAO**

> Katika uzazi wa mtoto wake wa pili alifuata maelekezo aliyoyapata kutoka kwa wataalamu wa afya na hakuugua kama wa mwanzo.

### MAMA ALIYEJIFUNZA

Ushahidi wa uelewa huo unatoka kwake, Agnes James, mkazi wa kitongoji cha Bubalebwela, katika kijiji cha Kilimilile, wilayani Missenyi, alipozungumza na Nipashe wiki kadhaa zilizopita, wakati huo mwanawe akiwa na wiki mbili tu duniani .

"Nilijifungua mtoto huyu akiwa hana nguvu. Aliwekwa kwenye mashine ya kumsaidia kupumua, lakini muda mfupi ndani ya saa moja, alirudishwa nikamnyonyesha, akanyonya," anasema.

Mama huyo anaeleza kufahamu umuhimu wa kunyonyesha mtoto ndani ya saa moja baada ya kujifungua, kutokana na elimu aliyoipata kwenye vituo vya kutoa huduma za afya na wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Anasema hata watoto wake wawili waliotangulia, aliwanyonyesha kwa kufuata utaratibu huo, ikiwa zao la elimu ya kutoka kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii na vituo vya kutoa huduma za afya.

Mama Agness anasema, aliipata elimu hiyo shuleni, sekondari hadi kidato cha nne na anaongeza: "Pia, tunaendelea kupata elimu kutoka kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya kupitia semina mbalimbali na mafunzo yanayotolewa Siku ya Mama na Mtoto. "

Aidha kuhusu kumnyonyesha mtoto miezi sita bila kumchanganyia vyakula vingine anasema alilizingatia hilo kwa watoto wake wote ambao anasema ni wenye afya njema.

"Mimi hata kliniki sijawahi kuitwa mbele na kuhojiwa kuhusu afya ya watoto wangu kama ninavyoona akina mama wengine wanaitwa na kubakizwa ili wapewe mafunzo zaidi namna ya kulisha watoto," anasema.

Agness, anasema kunyonyesha watoto inavyotakiwa kunamsaidia mengi, ikiwamo kupanga uzazi, maana alifundishwa kuwa mama anaponyonyesha mtoto inavyotakiwa, si rahisi kupata mimba.

Anawashauri kinamama wenzake kuzingatia wanayofundishwa na wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii na katika vituo vya kutoa huduma ya afya, ili kulinda afya za watoto wao.

### WATAALAMU LISHE

Sista Margaret Ishengoma, ni mtaalamu wa mabadiliko ya tabia katika lishe wa shirika la IMA World Health, chini ya Mradi wa 'Mtoto Mwerevu' unaofadhiliwa na serikali ya Uingereza.

Anasema mtoto akishazaliwa, anapaswa kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa muda wa miezi sita ya mwanzo.

" Mtoto huyu hapaswi kuchanganyiwa kitu chochote kile, hata kama ni maji ya kunywa, maana hakuna chakula chochote kinachoweza kuchukua nafasi ya maziwa ya mama," anasema.

Anaeleza kwamba, katika maziwa ya mama kuna virutubisho vinavyojenga ubongo wa mtoto na kumfanya kuwa mwerevu, mbunifu na asiyeshambuliwa na magonjwa.

"Baada ya miezi sita ya mwanzo, ndipo wazazi wanapaswa kuwapatia watoto wao chakula kingine cha nyongeza, lakini kiwe na virutubisho vinavyotakiwa, kutoka katika makundi matano ya vyakula, ikiwamo vyenye asili ya wanyama na mboga za majani," anasema.

Katika hoja hiyo, Mratibu Lishe katika Wilaya ya Missenyi, Zeinath Hassan, anasema mtoto kunyonya maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa ina umuhimu mkubwa.

"Maziwa ya mama ya mwanzo yenye rangi ya njano yana virutu-

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Kijue kinachogharimu wazazi wanaonyonyesha 'vichanga'

**INATOKA UK.19**

busho vyote vinavyotakiwa. Yana kinga inayosaidia kumwongezea kinga mtoto tangu anapozaliwa, maana huzaliwa bila ya kinga na hutegemea kinga ya mama yake," anasema.

Mratibu huyo anataja faida nyingine ya mtoto kunyonya maziwa hayo, ni kumsaidia kutoa kinyesi cha kwanza, hivyo asipoyanyonya, itamchukua muda mrefu kutoa kinyesi hicho na kumsababisha mtoto shida ya kiafya.

Anasema kuwa unyonyeshaji wa maziwa hayo, unachochea maziwa ya mama kuanza kutoka kwa wingi, na mama asipomnyonyesha anapata shida ya kupata maziwa.

"Watoto ambao hawajanyonyeshwa maziwa hayo, hushambuliwa zaidi na magonjwa na hupata homa za mara kwa mara. Hata mama aliyefanyiwa upasuaji, lazima mtoto awezeshwe kunyonya ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa," anasema.

Mratibu Zeinath anasisistiza kwamba ni muhimu mama kumnyonyesha mtoto ndani ya miezi sita bila ya kumchanganyia vyakula vingine kama maji, isipokuwa dawa alizoandikiwa na daktari.

"Maziwa ya mama ya miezi sita yana virutubisho ambavyo humtosheleza mahitaji mtoto, kwa ajili ya ukuaji na maendeleo yake," anasema.

Anasema, maziwa hayo yana kiasi kikubwa cha maji na kwamba asilimia 80 ya maziwa ya mama yanakuwa na maji na anasistiza: "Wanaosema wampe mtoto maji wakidai amepata kiu haikubaliki".

Zeinath anasema kwamba mtoto anaponyonya sana katika kipindi hicho, kunawezesha upatikanaji maziwa ya mama kwa wingi na katika taratibu za afya hairuhusiwi mtoto kuanzishiwa chakula ndani ya miezi sita.

Anasema, mtoto anapopewa chakula cha nyongeza katika kipindi hicho, kunaweza kusababisha kupewa lishe yenye virutubisho duni visivyofikia kiwango cha maziwa ya mama, hali inayomsababishia akose kinga.

Kwa mujibu wa Zeinath, maziwa ya mama yana kinga, yana chakula cha kutosheleza mahitaji kwa ukuaji wa mtoto na maendeleo yake kwa ujumla.

"Mtoto akianzishiwa vyakula vingine ndani ya miezi sita, inaweza kusababisha kushambuliwa na magonjwa mara kwa mara, maana atakuwa anakula chakula kisicho na virutubisho kama maziwa ya mama. Kwa hiyo, ataathirika katika masuala ya ukuaji wa kimwili na kiakili" anasema.

Mtaalamu lishe huyo anazidi kueleza kwamba kumpa mtoto vyakula vya nyongeza, kunaweza kumfanya mama aridhike kuwa mtoto wake ana afya nzuri, kuona kaongezeka uzito, lakini mtoto huyo ataathirika katika ukuaji, kwani atakuwa anakula chakula cha wanga.



Mkazi wa Minziro, wilayani Misenyi, akimnywesha uji mwanawe, baada ya kupata mafunzo ya upikaji lishe ya watoto. **PICHA: MTANDAO**

> **Mlezi anapaswa kuelezwa namna ya kuchemsha maji na kisha kuweka chombo cha maziwa ndani yake ili kuyapasha kidogo na kumnywesha mtoto. Cha muhimu ni kuhakikisha vyombo vinavyotumika vina usafi wa kutosha.**

Anasema kwamba, mama anapaswa kula chakula cha kutosha ili kuzalisha maziwa ya kumtosha kumnyonyesha mtoto usiku na mchana kwa miezi sita, bila ya kumpa vyakula vingine ili kuamsha vichocheo, lakini akimchanganyia vyakula, hatoweza kumnyonyesha ipasavyo na maziwa yatapungua.

"Vyakula vingine vinakuwa na ladha tofauti, mfano sukari au chumvi, vinaweza kumfanya mtoto asinyonye tena maziwa ya mama kutokana na kuonjeshwa ladha tofauti. Hii inaweza kumfanya kuendelea kula vyakula visivyo na virutubisho kulingana na umri wake," anasema.

Mratibu lishe huyo anataja athari nyingine zinazoweza kusababishwa na mtoto kulishwa vyakula vya nyongeza ndani ya miezi sita, ni kuugua kila mara magonjwa mbalimbali zikiwamo njia za hewa.

Anataja, kuna suala la kuhara kwa sababu ya vifaa au maji wanayokuwa wamempa yasipokuwa safi na salama, na kuathiri ukuaji mwili na akili.

Mratibu Lishe, anataja athari nyingine ni uhusiano wa mama na mtoto kupungua kutokana na kutonyonyeshwa, mama kupata ujauzito katika kipindi kifupi, maana anapokuwa ananyonyesha vichocheo vya kupevusha yai vinakuwa duni na kusababisha udumavu kwa mtoto.

"Asilimia kubwa ya watoto walioduma ni wale ambao hawakunyonya maziwa ya mama pekee katika kipindi cha miezi sita," anasema Zeinath.

Anasema kumnyonyesha mtoto miezi sita, bila ya kumpa vyakula vingine, kunamsaidia mama kurudi katika umbo lake la kawaida mapema, lakini mama huyo asiponyonyesha vizuri, anaweza kuchelewa kurudi katika umbo lake na kuchangia kuongezeka uzito.

Anasema, kinamama ambao ni watumishi katika ofisi tofauti wamekuwa wakishindwa kuwanyonyesha watoto wao inavyoelekezwa na kwa sasa miongozo inaendelea kutolewa, ili kuweka mazingira ya kuwawezesha watumishi, pia kuwanyonyesha watoto wao miezi sita bila kuwapa vyakula vingine.

"Katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza, mama anakuwa katika mapumziko ya uzazi. Miezi mitatu mingine mama anapewa muda wa ziada.

"Inabidi kufanya kazi kwa muda wa saa sita tu na kuruhusiwa kufika kazini akiwa amechelewa kidogo na anaruhusiwa kuondoka kabla ya muda," anafanua mtalamu huyo.

Angalizo hilo pia liko kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004

### KUHIFADHI MAZIWA

Zeinath anasema, bado wanaendelea kuwahamasisha kinamama kukamua maziwa kwa ajili ya watoto wao wachanga, kwani yanaweza kuhifadhiwa katika vifaa safi na yana uwezo wa kukaa saa nane kwenye hali ya kawaida.

"Mlezi anapaswa kuelezwa namna ya kuchemsha maji na kisha kuweka chombo cha maziwa ndani yake ili kuyapasha kidogo na kumnywesha mtoto. Cha muhimu ni kuhakikisha vyombo vinavyotumika vina usafi wa kutosha," anasema na kuongeza:

"Lakini maziwa hayo yakizidi saa nane, itabidi yawekwe kwenye jokofu, yakiwa humo yanaweza kukaa saa 36 yakiwa bado yana viwango vile vile vya kawaida.Kwa hiyo, hakuna kizuizi cha mtoto kutotumia maziwa ya mama pekee hata akisafiri siku mbili."

Anashauri mbinu bora ya kuyaendeleza yatoke, ni kwa mama kuyakamua maziwa hayo, ili kuzuia uzalishaji wake usipungue wakati amesafiri.

### CHANGAMOTO

Mratibu huyo anaeleza changamoto za kimila na desturi zinazomdai binadamu hawezi kukamuliwa maziwa, zimepitwa na wakati, kwani baadhi ya watumishi waliokamua maziwa yao na kuwanywesha watoto baadaye ni mashuhuda wa uwezekano huo.

Anataja changamoto nyingine ni kinamama imnapotolea wanawaza sana mambo mengi, katika kipindi cha unyonyeshaji, imnachangia maziwa kutopatikana kwa wingi.

"Kinamama wengine hawapati chakula cha kutosha katika kipindi cha unyonyeshaji, hivyo tunaendelea kuhamasisha mama anayenyonyesha apewe msaada kwenye jamii ili apate chakula cha kutosha na muda wa kupumzika," anasema.

Anasema pia wanaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 154 katika Kata zote 20 zilizoko katika wilaya ya Missenyi, ambao hutembelea kaya na kuhamasisha jamii umuhimu wa unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo.

"Tunaelimisha pia kuhusu umuhimu wa ushiriki wa akina baba katika malezi ya mtoto, lakini pia elimu hii mbali na kupitia kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, pia inatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya, kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa," anasema.

Zeinath anasema kinamama wengi wameanza kuelewa umuhimu huo na kwamba asilimia 46 ya kinamama, hivi sasa wanannyonyesha kwa kufuata taratibu za unyonyeshaji, ikilinganishwa na siku za nyuma wachache walioitikia wito huo.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef) na kuzinduliwa mwishoni mwa mwaka jana, asilimia 59 ya watoto wenye umri chini ya miezi sita walinyonyeshwa maziwa ya mama pekee nchini.



HABARI MBEYA

# Ahadi ya serikali kilimo parachichi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imesema inakusudia kuimarisha kilimo cha maparachichi ambayo yana soko kubwa kimataifa ili kuongeza kiwango cha uuzaji wa bidhaa nje ya nchi utakaosaidia kuongeza pato la taifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philipo Mpango, alipokuwa kwenye ziara wilayani Rungwe pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwekezaji, Angela Kairuki, kutatua changamoto za wawekezaji wa zao hilo.

Dk. Mpango alisema moja ya kigezo cha kukua kwa uchumi ni namna nchi husika inavyouza bidhaa zake kwenye soko la kimataifa, hivyo akasisitiza kuwa parachichi ni miongoni mwa mazao yatakayoifanya Tanzania kufikia hatua hiyo.

Alisema wawekezaji wakubwa wa maparachichi katika Wilaya ya Rungwe yaani makampuni ya Rungwe Avocado limited Cuser Africa Limited, yameleta fursa kubwa ambayo wananchi wanatakiwa waitumie kuinua uchumi wao na wa taifa.

"Serikali imekusudia kuinua uchumi wa taifa, sasa tumekuwa tukiuza sana korosho, tunataka zao la parachichi liwe miongoni mwa mazao tunayouza nje hivyo tunawahamasisha wananchi waitumie vizuri fursa hii," alisema Dk. Mpango.

Kwa upande wake, Kairuki alisema ofisi yake inawakaribisha wawekezaji wengine kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza ushindani.

Alisema kutokana na umuhimu wa kilimo katika ukuaji wa uchumi wa taifa, anamuomba Waziri wa Fedha kutenga bajeti za kutosha kwenye kilimo ili kuimarisha uwekezaji kwenye sekta hiyo muhimu.

Alisema baada ya kumaliza mgogoro wa wawekezaji wa makampuni mawili yaliyokuwa yanasigana kwa muda mrefu, wananchi watanufaika zaidi kutokana na kuuza mazao yao kwa bei nzuri.

"Nashukuru kwa kuwa tumekuja na Waziri wa Fedha huku, ameshuhudia uwekezaji mkubwa sana sasa naamini wakati wa bajeti atatutengea fedha za kutosha ili uwekezaji wetu uwe na tija zaidi," alisema Kairuki.

Kairuki alisema wakati serikali inahangaika kuwashawishi wawekezaji kuja kuwekeza ni lazima yawapo mazingira ya kuwashawishi ili waje wawekeze ikiwemo miundombinu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Godfrey Mwambe, alisema ofisi yake iko tayari kumpokea mwekezaji yeyote ambaye atakuwa mwenye faida kwa wananchi wa Tanzania.

Alisema wawekezaji wa maparachichi katika Wilaya ya Rungwe wakati wanasuguana waliokuwa wanaumia ni wakulima wa kawaida ambao walikuwa wanaelekea kukosa soko la mazao yao.

Alisema wanahitajika wawekezaji wengi ili kuongeza ushindani wa bei na kupelekea kupanda kwa bei ya maparachichi na hivyo kuwanufaisha zaidi wakulima wadogo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango aliagiza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa andiko la kisheria la makubaliano ya wawekezaji hao kumaliza tofauti zao.

Alisema baada ya andiko hilo kukamilika, wawakilishi wa makampuni hayo wataitwa Dar es Salaam ama Dodoma kwenda kusaini makubaliano hayo.

# Atiwa mbaroni kwa tuhuma za kumnajisi binti wa kumzaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa wilaya ya Kyela mkoani hapa, amekamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumnajisi binti yake.

Mtuhumiwa huyo ajulikanaye kwa jina la Samwel Msukila (22) mkazi wa Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, anashikiliwa na Jeshi hilo kwa tuhuma za kumbaka mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka tisa.

Hayo yalibainishwa jana na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Ulrich Matei, akizungumza na wanahabari, na kwamba kijana huyo alitenda unyama huo Februari 16 mwaka huu majira ya saa 2:00 usiku.

Matei alisema kwamba taarifa zilifikishwa katika Kituo cha Polisi Februari 19, kisha mtuhumiwa akakamatwa na kuwekwa mahabusu wakati taratibu zingine zikiendele.

Alisema mtuhumiwa huyo alimchukua mtoto wake huyo ambaye anasoma darasa la tatu na kwenda naye kwenye shamba la mahindi kisha akambaka.

Hata hivyo Kamanda Matei alisisitiza kuwa matukio yote mawili na mengine ambayo yamekuwa yakitokea mkoani humo hayahusiani na imani za kishirikina na badala yake ni tamaa za kimwili za wahusika.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa jeshi la Polisi kila wanapowabaini wabakaji na waharifu wengine ili kuhakikisha wahusika wanakamatwa na vitendo hivyo vya unyanyasaji wa watoto vinakoma.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akisaka wateja wa kizimba cha kufugia samaki wa mapambo katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Morocco, jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Watendaji kusakwa ubadhirifu fedha hospitali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

UONGOZI wa Wilaya ya Mbarali, umeagizwa kuwasaka na kuwakamata kisha kuwachukulia hatua za kisheria watendaji wote wa Halmashauri hiyo waliohusika na ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa Hospitali ya wilaya hiyo.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kanali Ngemela Lubinga, alipokuwa ziarani wilayani humo ambapo alitembelea mradi wa hospitali hiyo na mingine ikiwamo ya maji ambayo watendaji wanadaiwa kuchakachua fedha.

Kanali Lubinga alisikitishwa na taarifa za upotevu wa nyaraka mhimu za ujenzi wa jengo la Hospitali hiyo ambazo hazijulikani zilipo.

Alimpongeza Mkuu wa Wilaya hiyo, Reubein Mfune, kwa kuchukua hatua za kuagiza Takukuru kufanya uchunguzi wa ujenzi wa jengo hilo na kwamba watakaobainika wachukuliwe hatua.


Alisema atawasiliana na Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, ili wahusika wakamatwe popote walipo hata kama wapo nje ya Mbarali.

Alisema haiwezekani serikali inahangaika kutafuta fedha za miradi halafu watu wengine wachache wanajinufaisha nazo.

Mfune alisema Jengo la Hospitali hiyo ya Wilaya lilianza kujengwa mwaka 2010 lakini kukawa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa lilijengwa kwa gharama kubwa kuliko uhalisia wake.

Alisema kutokana na malalamiko ya wananchi hao ambao baadhi walikuwa wanadai jengo hilo haliendani na thamani ya fedha zilizokuwa zinatajwa na wengine kudai limejengwa chini ya kiwango, aliamua kuunda tume ya uchunguzi ambayo inaendelea na kazi.

Alisema miongoni mwa vitu ambavyo Tume hiyo inafuatilia ni matumizi ya fedha kulingana na taratibu za manunuzi ya Serikali na ubora wa jengo hilo ili kujua usahihi wa matumizi ya fedha.







Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu (kushoto), akiongoza kikao kilichokutanisha menejimenti ya wizara na wadau kutoka mashirika ya C-SEMA na SOS-Children Village Tanzania, kujadili jinsi ya kuweka mikakati madhubuti katika kuwezesha ongezeko la bajeti katika masuala ya watoto nchini, kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: WAMJW**

# Jafo atangaza neema kwa wakutubi bajeti ijayo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema katika bajeti ijayo ya 2019/20, wanatarajia kutoa ajira kwa kada ya wakutubi katika maktaba za shule za msingi na sekondari nchini.

Amesema nia ya kufanya hivyo ni kuwawajengea wanafunzi tabia ya kujisomea vitabu.

Jafo aliyasema hayo jana wakati alipokuwa akifungua semina pamoja na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Chama cha Wakutubia nchini (TLA), unaofanyika jijini Dodoma kwa siku tatu.

Alisema kuwa taaluma ya ukutubi nchini imekuwa haipewi thamani na watu wengi pamoja na kuwa ndiyo sehemu muhimu inayo hifadhi maarifa mbalimbali.

Aidha, alisema kutokana na umuhimu wa wakutubi katika maktaba mbalimbali serikali kupitia Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tamisemi, itafanya tathmini ya idadi ya wakutubi waliopo pamoja na maktaba ili kuweza kubaini changamoto iliyopo katika sekta hiyo.

"Katika bajeti ijayo tutajitahidi ili tuajiri wakutubi katika shule zetu za msingi pamoja na sekondari takribani shule 17,000 nilizonazo ili tupate wataalamu wenye weledi wa mambo ya maktaba na kuacha tabia ya kutumia walimu wa kawaida katika sehemu hiyo,"alisema Jafo. Vilevile, alisema kuwa serikali inao mpango wa kuboresha shule kongwe pamoja na maktaba zake ambazo hivi sasa zipo katika hali mbaya.

"Sasa hivi tunafanya uboreshaji wa maktaba zetu katika shule zote kongwe nchini, lakini hili litakwenda sambamba na suala la kuajiri wakutubi wenye taaluma husika, ili kuweza kuwajengea uwezo wanafunzi katika kujisomea," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakutubi nchini Dk. Juliana Manyerere, alisema kuwa chama hicho kimetimiza miaka 46 tangu kianzishwe na lengo lake ni kuhamasisha matumizi ya maktaba.

Aidha, Dk. Manyerere, aliomba serikali kuweka msisitizo katika matumizi ya maktaba kwa shule za msingi na sekondari nchini.

"Katika kuboresha elimu yetu vimekuwa vikitajwa vitu vingi ikiwamo maabara, madawati, lakini maktaba hazitajwi sana lakini ukweli ni kwamba tukiwa na maktaba katika shule zetu watoto wataweza kujipatia maarifa kupitia vitabu mbalimbali watakavyokuwa wanasoma," alisema.

# Dodoma kuongeza madarasa na maabara

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imetenga Sh. bilioni 2.7 kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa na maabara.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alipozungumza na waandishi wa habari kwenye ziara ya kukagua miundombinu ya madarasa kwa baadhi ya shule za sekondari.

Kunambi alisema fedha hizo zimetengwa kwenye bajeti ya 2018/19 na zimeshaanza kujenga vyumba vya madarasa na maabara kwa baadhi ya shule za sekondari jijini hapa.

Aidha, alisema halmashauri hiyo iliweka malengo ya kukusanya Sh. bilioni 68, lakini mpaka sasa wamefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 46.

"Katika mapato haya tayari vyumba 15 vya maabara vimeanza kujengwa katika baadhi ya shule za sekondari na malengo ni kukamilika ifikapo Machi mwaka huu,"alisema.

Hata hivyo, Kunambi alisema mahitaji ya vyumba vya maabara ni 111, lakini kutokana na bajeti wanaendelea kutumia fedha hizo kwa ajili ya kujenga vyumba zaidi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Dodoma, Mwalimu Amani Mfaume, alisema shule hiyo ilipokea Sh. milioni 150 kutoka mfuko wa EP4R kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mfaume alisema ujenzi wa mabweni hayo ulianza mwenzi Machi mwaka jana, baada ya kupitia taratibu zote ikiwa ni pamoja na kuijulisha bodi na utoaji matangazo huku bweni moja likigharimu Sh. milioni 75.

Aidha, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliwapatia Sh. milioni 120 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa mabweni hayo yaliyopo ndani ya eneo la shule na hivyo ujenzi wa mabweni hayo kufikisha zaidi ya Sh. milioni 270.

Alisema ujenzi wa bweni la kwanza umekamilika kwa asilimia 99, huku bweni la pili ujenzi wake ukiwa umefikia asilimia 87.

# 357 wakosa makazi Chamwino

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

FAMILIA 357 za kijiji cha Machali B, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, zimekosa makazi kutokana na nyumba zao kuezuliwa na upepo mkali ulioambatana na mvua ya mawe. Akizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Ladlaus Lumboto, alisema nyumba hizo zimeezuliwa juzi na kwamba familia hizo zimehifadhiwa na majirani na zingine ziko kwenye jengo la zahanati.

"Nyumba hizi zimeezuliwa na upepo, hakuna nyumba hata vyakula vyao vimelowana na mvua hali ambayo imesababisha kukosa chakula, kuna nyumba za ibada nazo zimekumbwa na adha hii,"alisema. Ofisa Mtendaji huyo alisema bado wanaendelea kufanya ukaguzi zaidi ili kuona kama kuna majanga zaidi ya hayo kwa ajili ya kutoa misaada muhimu itakayohitajika kwa familia.

"Hata hivyo pamoja na hasara iliyojitokeza kwenye familia hizi, tunamshukuru Mungu hakuna tukio lolote lililosababisha kifo au kujeruhi kwasababu watu wote wako salama, zaidi ni chakula tu kilicholowana na mvua," alisema. Mmoja wa waathirika wa mvua hizo, Oripha Mazengo (60), aliomba serikali kusaidia kuzijengea nyumba za familia ambazo uwezo wake wa kurejesha makazi ni mdogo.

"Baadhi ya waliopatwa na majanga haya hawana uwezo wa kurejesha mabati kwenye nyumba zao kutokana na maisha yao kuwa ya kimaskini, hivyo tunaomba serikali itusaidie katika hili," alisema.



# Shein aja juu michango shuleni

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema haifai wanafunzi kuwekewa vikwazo vya kusoma kwa kutoza fedha ili kuchangia huduma za elimu.

Alisema serikali ina uwezo wa kutosha kushughulikia huduma za elimu bila malipo, ili kuwawezesha watoto wa wanyonge kufaidi matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliyasema hayo baada ya kuweka jiwe la msingi kwa ujenzi wa Shule ya Maandalizi na Msingi Uzing'ambwa katika Jimbo la Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

Katika hatua nyingine, Dk. Shein aliwataka wananchi wa kijiji hicho, kuacha biashara ya magendo, ambayo alisema inaikosesha mapato serikali.

Dk. Shein alikopongeza Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa kazi nzuri inayoifanya, akisema watu wamekuwa wakifanya makosa kwa kusafirisha bidhaa kama vile unga, mchele, sukari na mafuta bila ya kufuata taratibu na sheria za nchi. kuhusu barabara ya Unguja Ukuu-Kaepwani hadi Uzi, Rais alisema serikali ina mpango wa kuijenga kwa lami ili kuwaondoshea usumbufu wananchi, sambamba na kujiandaa kujenga daraja na kuifanya ipitike wakati wote.

Alisema serikali anayoiongoza itahakikisha inaimarisha huduma za maendeleo ikiwamo kujenga barabara na daraja katika kijiji hicho ambacho kimezungukwa na bahari.

Alieleza kuwa serikali ina mipango kabambe ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma zote muhimu kwa uhakika ikiwamo usafiri wa barabara, shule ya sekondari pamoja na kuimarisha huduma za majisafi na salama.

Akiwa katika majumuisho ya ziara yake hiyo pamoja na mazungumzo na viongozi wa CCM wa Wilaya ya kati Mkoa wa Kusini Unguja, aliwasisitiza viongozi wa wilaya hiyo kuzigeuza changamoto chache zilizoko kuwa mafanikio kwa kufanya kazi kwa pamoja na kwa ushirikiano.

Sambamba na hayo, Dk. Shein alieleza changamoto ya wizi wa mazao, wizi wa kuvunja nyumba ambao alisema ni miongoni mwa mambo ya uhalifu yaliyomo katika wilaya hiyo ambayo yanahitaji kukomeshwa.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe (wapili kulia), akikabidhi hati ya kijiji kwa mkazi wa Msomelea, Josephina Ng'anga, wakati wa hafla fupi iliyofanyika kijijini hapo hivi karibuni. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Madaktari ruksa kufanya kazi vituo binafsi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema madaktari na wasaidizi wake wapo huru kufanya kazi zao za kutoa huduma za afya katika vituo binafsi baada ya muda wa kazi.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, wakati akijibu swali la nyongeza la Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua kama madaktari kufanya kazi katika hospitali za binafsi ni sahihi. Naibu waziri huyo alisema si dhambi kwa watumishi katika sekta ya afya kuanzia madaktari na wasaidizi wao baada ya kufanya kazi za kutoa huduma za afya kutumia muda wa nyongeza kazi binafsi.

Alisema hatua hiyo kwa kiasi kikubwa inawasaidia madaktari hao kupata kipato cha ziada na kusaidia kuendesha maisha yao.

"Mheshimiwa Spika, hakuna tatizo kwa madaktari na wasaidizi wao katika sekta ya afya kufanya kazi za ziada katika hospitali binafsi, kwa kuwa hiyo itasaidia kuongeza ujuzi na mapato," alisema. Aliwakumbusha wafanyakazi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwambawanaongeza ufanisi na kuleta tija kwa kutoa huduma bora za matibabu kwa wananchi.

Alisema dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ni kutoa matibabu bure kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kufikisha huduma muhimu kwa wananchi katika sekta ya afya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa ugatuzi," alisema.

# Serikali kudhibiti bei bidhaa muhimu

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Biashara na Viwanda, Mohamed Hafidh Khamis, amesema serikali itaendelea kudhibiti bei ya bidhaa muhimu za vyakula ikiwamo mchele na unga wa ngano kwa ajili ya kuleta unafuu wa wananchi wake.

Khamis alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, Suleiman Said Sarhani, aliyetaka kujua kwa nini wafanyabiashara wanapandisha bei ya bidhaa wanavyoopenda wakati bidhaa nyingine muhimu zimepunguzwa ushuru.

Alisema serikali inatekeleza sera ya biashara huria ambayo wafanyabiashara ndiyo waagizaji wa bidhaa muhimu za vyakula na nyinginezo.

Alisema zipo baadhi za vyakula muhimu zitaendelea kudhibitiwa na serikali ambazo zimepunguziwa ushuru ili kutoa unafuu kwa wananchi kupunguza ukali wa gharama za maisha.

Alizitaja bidhaa zilizosamehewa ushuru kwa kupunguzwa kutoka kwa wafanyabiashara ni mchele ambacho ni chakula muhimu kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na unga wa ngano na sukari.

"Mheshimiwa Spika, serikali inafuatilia kwa karibu sana bei ya bidhaa muhimu za vyakula na kuona hazipandishwi kiholela ikiwamo mchele, unga wa ngano pamoja na sukari," alisema.

Hata hivyo, aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali imeunda tume halali ya kumlinda mlaji sheria namba 8 ya mwaka 2018, kwa ajili ya kudhibiti mwenendo wa bei za vyakula.

Alisema licha ya kuwapo kwa mfumo wa biashara huria, tume ya kumlinda mlaji ni chombo cha serikali ambacho miongoni mwa majukumu yake ni kuangalia mwenendo wa bei za vyakula.

Alieleza kuwa hakuna sababu ya wafanyabiashara kuongeza bei juu ya bidhaa muhimu za vyakula kwa sababu bidhaa hizo zimepunguziwa ushuru ili kutoa unafuu kwa wananchi.

"Mheshimiwa Spika, mimi sioni sababu ya wafanyabiashara kupandisha bei juu ya bidhaa muhimu ikiwamo mchele, unga wa ngano pamoja na sukari kwa sababu bidhaa hizo tumepunguza ushuru wake ili zitoe nafuu kwa wananchi wetu," alisema.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 Feb**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Delirious
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 24 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesliga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Kisasi cha utata
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)









## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

## Tume ya uchaguzi Nigeria matatani

**LAGOS, Nigeria**

MVUTANO mkali umeendelea kati ya vyama vikuu vinavyoshutumiana kutaka kuvuruga uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika kesho kutwa, huku mashirika ya kiraia yakijiuliza kuhusu hatima ya Tume ya Uchaguzi (INEC).

Wananchi wengi nchini humo wanajiuliza kuhusu hatima ya INEC baada ya kuchukuwa hatua ya kusogeza mbele uchaguzi.

Uchaguzi uliotarajiwa kufanyika Februari 16 uliahirishwa kwa juma moja hadi Februari 23 hali iliyowashangaza wananchi wengi.

Mkurugenzi wa shirika linalofuatilia na kutetea demokrasia na Maendeleo Nigeria, Idayat Hassan alisema siyo mara ya kwanza kwa INEC kuhairisha uchaguzi.

"Imekuwa sasa ni tabia mbovu tangu mwaka 2011. Mwaka huo, uchaguzi ulisitishwa mchana. Mwaka 2015, uchaguzi mkuu ulisogezwa mbele, kwa sababu ya tatizo la usalama. Na mwaka huu tena, zikisalia tu saa 5 kabla ya kuanza zoezi la kupiga kura, uchaguzi umeahirishwa, Yote haya yanachafua taifa hili, " alisema Hassan.

*RFI*

## Rais wa Somalia ziarani Burundi

**BUJUMBULA, Burundi**

RAIS wa Somalia, Mohamed Abdullahi Mohamed yupo ziarani nchini Burundi.

Akiwa nchini humo amesema nchi zilizopeleka wanajeshi kusimamia amani Somalia zitakuwa sehemu ya historia ya nchi yake.

Kwenye mazungumzo ya ana kwa ana na Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi , Rais Mohamed alisema anapendelea ufanyike mkutano wa haraka wa wakuu wa nchi zilozo na wanajeshi nchini Somalia, baada ya Umoja wa Afrika (AU) kuchukua uamuzi wa kupunguza wanajeshi 1,000 wa Burundi nchini mwake.

Alisema ziara yake nchini Burundi imedhamiria kutowa shukrani za thati kwa serikali ya nchi hiyo kwa kazi nzuri inayofanywa na wanajeshi wake wanao hudumu katika kikosi cha kusimamia amani Somalia.

Mwanasiasa huyo anayeongoza moja ya mataifa yenye hali dhaifu kabisa ya usalama duniani amesifu mchango uliotolewa na mataifa ya Afrika kwa kuchangia wanajeshi kwenye mpango wa kulinda amani nchini mwake, na ametaja mchango huo ni ishara kamili ya uwezo wa bara hilo kutatua matatizo yake yenyewe. Kwa upande wake Rais Pierre Nkurunziza alisema majadiliano yake na Rais Mohamed Abdullahi wa Somalia yamehusu juu ya kuimarisha uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili.

*DW*

# Amtorosha mwanawe hospitali kukwepa gharama

**NAIROBI, Kenya**

"NILIJARIBU kuchangisha fedha lakini nikaona kwamba kila ninapoendelea kuchangisha fedha ndipo gharama za matibabu hospitalini zinazidi, ndipo nikapata wazo la kumtorosha"

Ni kauli ya Boniface Murunge baba wa mtoto mchanga wa mwezi mmoja akisimulia wakati alipokamatwa na maofisa polisi baada ya kumtorosha mtoto wake aliyekuwa akipatiwa matibabu katika hospitali kuu ya Kenyatta jijini Nairobi.

Murege na mke wake Agness Elewo wanaishi kwenye chumba kimoja Ole Kasasi eneo la Ongata Rongai.

Elewe alilazwa katika hospitali kuu ya Kenyatta jijini Nairobi pamoja na mtoto wake mchanga wa mwezi mmoja aliyekuwa anasumbuliwa na tatizo la kushindwa kupumua vizuri, sambamba na joto la mwili kuwa juu.

Murege aliingiwa na hofu na hakuweza kufikiria kwamba mke wake na mwanawe wa kike walikuwa wamezuiliwa katika hospitali hiyo ya umma kwa sababu ya kushindwa kulipa gharama za malazi.

Murege ambaye alikuwa na kawaida ya kumtembelea mke wake hospitalini hapo kwa kumpeleka uji kama chakula cha kila siku kwa muda wa siku 21.

Inaelezwa kuwa Murege ndiye alimshawishi mke wake kuhusu njama ya kutoroka ili kukwepa kulipa gharama ya matibabu iliyofikia Ksh.56, 937 walizokuwa wanadaiwa.

"Mimi ni mfanyakazi na ninalipwa dola tano kwa siku ama saa nyingine ninakosa kabisa, ", alisema Murage

Mtoto huyo alilazwa tangu Januari 26 na alitarajiwa kutoka Februari 11, na gharama ya kulazwa ilikuwa Ksh.46, 000.

Marafiki Murage, majirani, na wafanyakazi wenzake walifanikiwa kuchangisha kiasi cha Ksh.2, 000, ikiwa ni kiwango kidogo zilizokuwa zikihitajika.

Anasema ndipo alipopata wazo la kumtorosha mtoto wake ili kuepuka gharama ambazo zilikuwa zikiongezeka kila siku.

"Na baadaye nikapata wazo hili: Kwa nini nisimuweke mtoto ndani ya begi na kuondoka katika hospitali hiyo.? Hakuna mtu atakayenigundua," alisema Murege na kuongeza.

"Niliendа hospitali nikamkuta mtoto amelala, hata sikuona kitu kingine cha kumwambia mke wangu. Nilimuuliza Wangechi anaweza kutosha hapa? Akaniambia ndio anaweza kutosha ndani ya begi nililokuwa nimebeba, nikamwambia tumuweke ndani yake akiwa amelala twende nyumbani".

Mke wake alijuwa matatizo ya kifedha ya mumewake hivyo hakukataa pendekezo la mumewe.

Muda mfupi badaye, Murage alibeba begi hilo ambalo aliweka tundu ili kumzuia mtoto huyo kutokosa hewa na mkewe akamfuata nyuma.

Ghalfa wakiwa njiani kutoka nje ya hospitali hiyo, alisimamishwa na walinzi waliomtilia shaka.

Murage alikaidi kusimama lakini walinzi hao waliwaita maafisa wa polisi kwa sababu waliamini alikuwa ni njama za kumuua mtoto huyo.

"Wakati natoka nilisimamishwa na mlinzi akaniuliza ni nini nilichokuwa nimebeba nikasema ni vyombo vya kubebea chakula, akasema hebu nione ndipo akamkuta mtoto, nikamwambia nimeshindwa kulipa gharama ya hospitali", alisema Murage.

Murage alikamatwa na maafisa wa polisi na kufungiwa katika chumba cha mahabusu, mkewe alisalia amezuiliwa katika hospitali hiyo.


Murage aliwaambia maafisa hao ukweli, hata hakimu wa mahakama ambayo alikuwa amepelekwa.

"Kwa kweli sikujua ni wapi kwingine ningetafuta usaidizi, nilikuwa nimeshindwa na niliamua kuomba kwamba njama hiyo ya kutoroka hospitalini ingefanya kazi", alisema Murage.

Alipofikishwa kwa hakimu mkuu mkazi, Caroline Nzibe, hakujua kwamba mkewe alikuwa ameachiliwa na gharama hiyo ya kulazwa kulipwa.

Alipoulizwa na mahakama iwapo angethubutu kufanya makosa kama hayo tena, licha ya kupewa kifungo cha nyumbani cha miezi mitatu, Murage alikiri na kusema kuwa yeye sio muhalifu. Baada ya kuachiwa huru, Murage alisema anatamani kumuona mwanaye anakuwa daktari kwa lengo la kuwasaidia watu wenye shida ambao wapo katika hospitali hiyo.

*BBC*



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, ambaye anatarajia kugombea urais mwaka 2021. **PICHA: REUTERS**

## Rais Museveni kugombea urais kwa mara ya sita

**KAMPALA, Uganda**

CHAMA tawala nchini Uganda kimemteua Rais Yoweri Kaguta Museveni kuwa mgombea wake wa urais katika uchaguzi wa mwaka 2021.

Rais Museveni mwenye umri wa miaka 74 aliingia madarakani kwa mtutu wa bunduki mwaka 1986, atagombea urais kwa muhula wa sita.

Chama chake cha National Resistance Movement (NRM) kimekubali, katika kikao kilichoongozwa na Museveni jana na kuridhia Museveni aendelee kuongoza harakati na taifa mwaka 2021 ili kuondosha vikwazo vya mabadiliko na maendeleo.

Hata hivyo, wakati akigombea muhula wa tano wa madaraka mwaka 2016, alisema kuwa huo haukuwa muda muafaka kwake kuondoka madarakani kwani bado alikuwa na kazi ya kufanya.

Kugombea kwa Rais Museveni katika uchaguzi ujao unakuja baada ya kusaini kuwa sheria mswada ambao uliondoa ukomo wa urais wa miaka 75.

Hata hivyo, kupitishwa kwa muswada huo bungeni kuligubikwa na vurumai kubwa kutokana na kupingwa na wabunge wa upizani, hadi wabunge wa upinzani na maafisa usalama walipigana ngumi ndani ya bunge.

Mahakama ya Upeo ya Uganda mwezi wa Januari imeanza kusikiliza shauri la kupinga mabadiliko hayo ya sheria.

Rais Museveni ameshampandisha cheo mwanawe, Kainerugaba Muhoozi na kutoka Meja Jenerali na kuwa Luteni Jenerali, cheo ambacho ni cha pili kwa ukubwa zaidi jeshini.

Ndani ya miaka sita iliyopita, Jenerali Muhoozi amepanda vyeo mara tatu.

*BBC*

## Watumishi wa umma kuburuzwa kortini

**Na Mwandishi Wetu, BUNDA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kuanza mchakato wa kuwaorodhesha watumishi wa umma ambao hawajalipa kodi ya pango la ardhi hadi sasa ili wafikishwe katika mabaraza ya ardhi na nyumba.

Mabula alitoa agizo hilo jana katika ziara yake inayoendelea kwenye wilaya za Bunda na Serengeti mkoani Mara na Ukerewe mkoani Mwanza, wakati wa ziara yake kuhamasisha malipo ya kodi ya pango la ardhi katika Kanda ya Ziwa. "Ninyi watumishi wa serikali mnatakiwa kuwa wa mfano katika kulipa kodi za serikali, kwa sababu hatuwezi kwenda kudai wengine wakati sisi wenyewe hatujalipa kodi ya pango la ardhi. Kokote nitakapopita nataka majina ya watumishi ambao hawajalipa ili wafikishwe katika mabaraza," alisema.

"Mheshimiwa Rais anasimamia miradi mikubwa hapa nchini kama ule wa ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa bwawa la kufua umeme wa Mto Rufiji na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania. Miradi hii yote inategemea kodi na mapato ya ndani, hivyo ni lazima tumuunge mkono katika kulipa kodi hizi," aliongeza.

Akiwa wilayani Ukerewe, alipokea taarifa ya Ofisi Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Tewe Shabani, kuwa hadi sasa halmashauri yake imeshakusanya Sh. 41,288,175 wakati lengo ni Sh. milioni 100 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kiasi hicho kilichokusanywa ni sawa na asilimia 41.2.

Ofisa huyo alisema hadi sasa ilani 131 zenye thamani ya Sh. 54,446,550 za madai ya kodi ya ardhi zimesambazwa kwa wadaiwa ambao wameanza kupunguza madeni yao na mpaka sasa wameshalipa Sh. 3,100,700 na kubaki Sh. 51,345,850.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Mabula alishangazwa na ukusanyaji huo hafifu wa maduhuli ya serikali na kumwagiza ofisa huyo kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa kodi ndani ya mwezi mmoja kuanzia jana na aanze na watumishi wote wa serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe. Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa, Mabula aliagiza kuwapo kwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi atakayesimamia kesi hizo na kuzitolea hukumu kwa wadaiwa sugu walipa kwa wakati na kama hawatatekeleza, milki zao zitauzwa ili kulipwa deni hilo.

Akiwa wilayani Bunda, Mabula alimwagiza ofisa ardhi mteule kumfikishia majina ya maofisa wa halmashauri ya wilaya hiyo ambao wanadaiwa kodi ya pango la ardhi na hawajalipa hadi sasa wakati muda wa kulipa kwa hiari ulishaisha tangu Januari 31.

# Naibu Waziri ataka umeme wa REA Geita

**Na Lusungu Helela, GEITA**

MBUNGE wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, ameomba umeme kupitia mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Amesema anahitaji umeme katika jimbo hilo ambalo kata zake mbili za Kalangalala na Bombambili ziko mjini na maeneo mengine ni vijijini.

Pia Kanyasu ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, amemwomba Waziri wa Nishati, Medard Kalemani, kuharakisha usambazaji wa umeme wa REA katika maeneo yaliyopitiwa na umeme huo kwa vile tangu mradi huo ulipozinduliwa mwaka jana, kijiji kimoja tu katika jimbo hilo ndicho kimenufaika na mradi huo.

Kanyasu alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa umeme wa REA uliofanyika katika kijiji cha Ibanda katika Wilaya ya Geita, eneo ambalo linahesabika kuwa ni mtaa.

Akizungumza kabla ya kuzindua umeme huo, Dk. Kalemani alitaja sababu zilizoifanya Geita Mjini kuchelewa kupata umeme wa REA, kwa vile inahesabika kuwa ni mjini na mjini hakuna vijiji bali kuna mitaa.

"Sisi tuliambiwa tupeleke umeme kwenye vijiji na si kwenye mitaa. Mheshimiwa Kanyasu ndiye kapigania kutwambia kuwa hii si mitaa bali ni vijiji," alisema Kalemani.

Hata hivyo, Waziri Kalemani alimhakikishia Kanyasu kuwa vijiji 42 tayari viko kwenye mpango wa kuunganishwa na mradi wa umeme wa REA.

Katika hatua nyingine, Waziri Kalemani aliwaagiza makandarasi na wataalamu wote kuwa hakuna kuruka nyumba wala kubagua nyumba bali wahakikishe kila mhitaji anaunganishiwa umeme haraka iwezekanavyo.

Aidha, Waziri Kalemani alipiga marufuku kuwatoza wananchi wanaotaka kuunganishiwa umeme zaidi ya Sh. 27,000 na kutoa wito kwa mwananchi atayetozwa zaidi ya kiasi hicho atoe taarifa ili hatua kali dhidi ya wahusika zichukuliwe. Aidha, aliwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ya kuunganishiwa kwa gharama hizo kwa kuwa baada ya hapo itabidi walipie kulingana na taratibu za Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco).



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philipo Mpango (kushoto) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki (wa pili kushoto), wakimsikiliza Mkurugenzi wa kampuni ya Cuser Africa Ltd, Robert Cuser (kulia), akielezea namna anavyoandaa miche ya miparachichi, wakati wa ziara ya viongozi hao kusuluhisha mgogoro kati ya kampuni hiyo na Rungwe Avocado Ltd, mkoani Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mtoto aliyeanguka mtini aomba msaada

**Na Beatrice Shayo**

MWANAFUNZI Amos Gabriel, ambaye alipata ulemavu akiwa shuleni jijini Mbeya na kushindwa kutembea, anaomba msaada wa Sh. milioni nne ili kukamilisha safari yake ya kwenda India kwa matibabu.

Mwanafunzi huyo ambaye alikuwa anasoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Samora Michael, alianguka alipopanda juu ya mti kutafuta fimbo aliyotumwa na mwalimu wake Aprili 25, mwaka jana.

Ilielezwa kuwa mwanafunzi huyo alipotumwa fimbo na mwalimu wake aliikosa na baada ya hapo alilazimika kupanda juu ya mti ambako alianguka na kuteguka shingo, kuvunjika mikono na kupata matatizo katika uti wa mgongo hali ambayo imemsababishia ashindwe kutembea.

Akizungumza na Nipashe jana, mama wa mtoto huyo, Swaumu Seseme, alisema wamejulishwa kuwa gharama za matibabu nchini India ni Sh. milioni 26.

Alisema kwa msaada wa fedha walizochangiwa na wadau mbalimbali mpaka sasa zimefikia Sh. milioni 22, hivyo zimebaki Sh. milioni nne ili mtoto wake akapatiwe matibabu.

"Nilituma ripoti ya ugonjwa wa mwanangu katika hospitali India wakaniambia gharama zake ni Sh. milioni 26. Walikuwa wameshanipangia tarehe ya kufika ili matibabu yaanze Februari 24, mwaka huu, lakini kinachonikwamisha ni hiyo fedha bado haijatimia," alisema.

Aliwaomba wasamaria wema waweze kumsaidia mtoto wake apate matibabu kwa kuwa anapitia wakati mgumu kutokana na ugonjwa unaomsumbua.

Desemba 16, mwaka jana, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, wakati akimkabidhi msaada wa Sh. milioni 9.46 alisema tayari ofisi yake imeshatoa maelekezo mawili katika Mkoa wa Mbeya iundwe kamati kujiridhisha na suala hilo.

"Tukio hilo limeonekana kwenye mitandao na limewagusa watu wengi naomba jambo hili tuchukuliwe kama ajali nyingine lisiwe na tafsiri nyingine. Sisi serikali tupo pamoja na mwanafunzi huyu ili kuhakikisha anafikia ndoto yake aliyosema ya kuwa daktari," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**SHAMBA LA ACRE 2 LINAUZWA** liko kilometre 3 toka chanika mjini ,mtaa wa > zogo ally kata ya homboza wilaya ya kisarawe bei ni milioni 43. No ya cm ni 0653019311

## MAGARI/VIPURI

**LOOKING FOR TOYOTA** NOAH for hiring long term contract. price 30,000 - 40,000 per day. Please call 0627301010 for details.

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

*Uza Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MODEST BIAS PRIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 415 BPK SANLG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KMR/RB/1981/2019.**

115072402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BERGER PAINTS (T) LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T457 BPA aina ya TOYOTA(CRESTA).Yenye chassis namba GX1006128150 .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**TaarifayaPolisi:**
**OB/RB/28121/2019.**

215072002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**OTIENO OSORO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COROLLA yenye namba za usajili T 431 AMM .Chassis namba AE1105145525. Engine namba. 5AG676018.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DOM/TR/ RB/306/2019.

115072302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DOMITILA ANIZETI KIMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 215 ACN** aina ya TOYOTA HILUX .Yenye chassis namba **LN85001880,** Engine **2L2092591.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TaarifayaPolisi:
**MS/RB/1540/019.**

215072102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;42/2019
Ombi la **TEKLA VITUS DIMOSSO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PAULO HILLARY DIMOSSO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 18/02/2019.

215071902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;10/2019

Ombi la **RAJABU J.NIA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SAID JUMA WAZIRI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **30/01/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **08/01/2019.**

215071802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI SHAHIDI**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI WILAYA YA MOROGORO**
**MADAI NAMBA 21....2019.**
**Mdai: OMARI SHABANI LIBAGULA**
**ANAMDAI**
**Mdaiwa: SUMA JKT**
**Kwa: SUMA JKT WA NANENANE**
**Madai ya PESA TASLIM TSH. 2,000,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 28 mwezi 02 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.Siku ya Alhamisi.Kwa kutoa ushahidi dhidi ya madai hayo.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 20 mwezi 02 mwaka 2019.

115072502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;41/2019**

**Ombi la SHABANI MWINYIMVUA CHOTA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAJABU IDDI CHOTA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 18/02/2019.

115072602

*Kwa Habari Motomoto*
*usikose Gazeti lako la The Guardian*
*kila siku*
*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*au piga simu: 0767 223311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# VALVERDE
## APOTEZEA UKAME WA SUAREZ

**LYON, Ufaransa**

KOCHA Ernesto Valverde amesisitiza hana shaka kuhusu ukame wa mabao wa Luis Suarez wakati aliposhindwa kuifungia Barcelona ikitoka sare ya bila kufungana na Lyon kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, Suarez alikuwa kwenye kiwango cha juu kwenye nusu ya kwanza ya msimu huu, lakini ameshindwa kung'ara mbele ya goli wakati Barca ikitoka sare nne kwenye mechi zao tano za mwisho.

Suarez katika mchezo huo dhidi ya Lyon alikosa nafasi kadhaa za kufunga na sasa amecheza mechi tano mfululizo bila kuziona nyavu.

Lakini kocha wa Barca, Valverde hana shaka na hilo.

"Ningekuwa na hofu kama angekuwa hatengenezi nafasi za kufunga, maana yake hii ndio kazi ya mshambuliaji," alisemaa Valverde akiwaambia waandishi wa habari.

"Mara zote alikuwa na nafasi, anatengeneza nafasi za kufunga na pia alifanya kazi kubwa kwenye mchezo dhidi ya Lyon."

# Rodriguez aifungulia milango Real Madrid

**MUNICH, Ujerumani**

JAMES Rodriguez anaonekana kufungua mlango kwa timu yake ya Real Madrid baada ya kumaliza miaka miwili ya mkopo pale Bayern Munich kufuatia kubainisha ana kila kitu katika klabu ya Madrid.

Baada ya kuwa na wakati mgumu kwenye mji mkuu wa Hispania Madrid na kujiimarisha mwenyewe hapo kwenye dimba la Bernabeu, James alihamia Ujerumani msimu wa 2017/18 kucheza kwa mkopo Bayern na kuwa na kipengele cha kununuliwa kwa euro milioni 42.

Bado mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia hajawa kwenye kiwango kizuri, huku pia majeraha ya mara kwa mara yakimsumbua na hakuwa dimbani Novemba na Desemba.


Huku mkataba wake na Real Madrid ukiwa unamalizika mwaka 2021, inaonyesha ni wazi kwamba klabu yake hiyo haitamuongezea mkataba mpya.

"Mjini Madrid, nina kila kitu kama vile nyumba na watu wanaonipenda," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akinukuliwa na Gazeti la Marca.

"Tunatakiwa kuangalia nini kitatokea, lakini kwa wakati huu nina mkataba na Bayern Munich. Nataka kumaliza msimu na kuangalia nini kitatokea," aliongeza.

"Nawasiliana na baadhi ya wachezaji wa Real ambao ni marafiki zangu na wote tunakuwa na furaha." Majeraha yamemuathiri James tangu aliposajiliwa kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 80 kutua hapo Real kufuatia kushinda Kiatu cha Dhahabu baada ya Kombe la Dunia mwaka 2014.

Alianza msimu wake wa kwanza nchini Hispania chini ya utawala wa Carlo Ancelotti unabakia kuwa ndio bora zaidi kwa kufunga mabao 17 katika mechi 46 alizoichezea.



# Klopp: Pasi za mwisho Liverpool tatizo kubwa

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amelaumu kwa timu yake kushindwa kutengeneza pasi za mwisho wakati Liverpool ikitoka sare ya bila kufungana na Bayern Munich kwenye mechi ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Safu ya ushambuliaji ya Liverpool ilikuwa butu wakati wakilazimishwa sare na Bayern kwenye Uwanja wa Anfield katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-Bora.

"Tatizo lao lilikuwa ni ubora wa pasi zetu za mwisho na wapizani wetu walikuwa na ubora na pasi zao za mwisho zilikuwa na ubora," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini katika hali ile tulitakiwa kucheza kwa ubora zaidi na tulikuwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani, lakini pia wapizani wetu walikuwa kwenye kiwango bora zaidi kushinda sisi.

"Utakuwa mchezo mgumu wa marudiano kucheza na Bayern. Kama tungeshinda 1-0 usiku huu (juzi), pengine mambo yangeweza kubadilika."

Sadio Mane na Mohamed Salah wote walikosa nafasi ya kuifungia Liverpool, ambao walikuwa wanashuka dimbani kwa mara kwanza tangu Februari 9.

Lakini Klopp, ambaye timu yake itakutana na Manchester United Jumapili, alikataa kutumia mapumziko ya siku 10 kama kisingizio.

"Mapumziko ya siku 10? Inahusiana nini na pasi za mwisho? Unatakiwa kuangalia mchezo na kufikiria kuhusu mchezo, na sio kuandaa swali kwa sababu ya mapumziko ya siku 10," alisema.



HABARI MICHEZO

# WENGER AIPA NENO ARSENAL KUHUSU OZIL

**MONACO, Ufaransa**

MESUT Ozil anaweza kuwa katika "ukanda wa faraja" pale Arsenal baada ya kupewa mkataba mpya mwaka jana, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa 'Washika Bunduki' hao, Arsene Wenger.

Ozil alisaini mkataba wa miaka mitatu na nusu Februari mwaka 2018 ambao unamfanya alipwe pauni 350,000 kwa wiki na kuwa mmoja wa wachezaji bora wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani. Lakini licha ya kuwa mmoja katika kundi la manahodha wa Arsenal chini ya mrithi wa Wenger, Unai Emery, Ozil ameanza katika mchezo mmoja tu wa Ligi Kuu mwaka 2019.

Ozil aliachwa nje na hakusafiri na kikosi Arsenal kilichochapwa bao 1-0 na BATE kwenye mchezo wa Ligi ya Europa na pia wiki iliyopita alikuwa mchezaji asiyetumiwa wakati wakifungwa 3-1 na Manchester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Na Wenger alihoji motisha ya Ozil huku akidai kwamba ingeigharimu klabu hiyo pauni milioni 100 kununua mchezaji wa kumrithi mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani.

"Ninaona kwamba urefu wa mkataba hauna kitu cha kufanya kawaida na uteuzi wa timu. Lakini wakati mwingine kuna matukio maalum," alisema Wenger katika tuzo za Laureus Jumatatu, ambapo alitunukiwa tuzo ya heshima.

"Mara nyingi tunadhani tunaposaini mchezaji kwa miaka mitano tuna mchezaji mzuri kwa miaka mitano, lakini hiyo haina maana kwamba wao hufanya kazi, wanacheza vizuri zaidi kwa sababu wanaweza kuwa katika eneo la faraja.

"Ana mkataba, lakini tatizo ni kwamba ikiwa unataka kununua mchezaji kama yeye unatumia pauni milioni 100. Na kudumisha thamani ya mchezaji kama Ozil ni ngumu."

# Deschamps amtetea Sarri nafasi ya Kante

**MONACO, Ufaransa**

UAMUZI wa kocha Maurizio Sarri kumtumia N'Golo Kante kama winga badala ya kiungo mkabaji pale Chelsea ni jambo zuri kwa sababu inasaidia timu kutanua wigo mpana, kwa mujibu wa kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps.

Baada ya kuanza vizuri msimu huu, kiwango cha Chelsea kimeshuka ghafla na wamevutwa hadi nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, wakati awali walionekana kutoa changamoto kubwa kwa Manchester City na Liverpool katika mbio za ubingwa.

Jorginho aliyesajiliwa msimu huu ameonekana kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Sarri, ambapo wawili hao walikuwa pamoja kule Napoli, na kocha huyo amekuwa akimtumia kiungo huyo wa Italia kwenye safu ya kiungo mkabaji na kumbadilisha Kante kuwa kiungo mshambuliaji.

Ingawa mabadiliko hayo yalionekana kufanya kazi vizuri hapo mwanzo, lakini katika wiki za hivi karibuni kiwango cha Jorginho kimeshuka na wengi wamemtaka Sarri kumshusha Muitaliano huyo na kumrejesha Kante katika nafasi yake ya awali.

Deschamps amekuwa akimtumia mchezaji huyo wa zamani wa Leicester City kama kiungo mkabaji, ingawa anaamini kuwa Kante atanufaika kwa kucheza nafasi tofauti.

"Inatokea kwa wachezaji wengine pia. Nimeona kocha (Sarri) kupendelea kumtumia kwenye nafasi nyingine kwa sababu ana mchezaji mwingine, Jorginho, ambaye anacheza kwenye nafasi ya kiungo mkabaji," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari katika tuzo za Laureus mjini Monaco.

"N'Golo Kante ana uwezo wa kucheza nafasi tofauti tofauti. Ni mchezaji wa kisasa, kiungo mzuri. Wakati akiwa na mimi kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa namtumia kama kiungo mkabaji.

"Ni muhimu zaidi kwenye ukabaji na kuichezesha timu. Kila kocha ana mfumo wake na mtazamo tofauti, lakini sihofii kuhusu hilo.

"Mara zote ni jambo zuri mchezaji kuwa na nafasi tofauti tofauti za kucheza uwanjani katika mifumo tofauti."



# DE GEA

## ATAKA PAUNI MIL. 90 KUBAKI UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inahofia golikipa, David de Gea anataka zaidi ya pauni milioni 90, ili asaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia kwenye timu hiyo.

Mkataba wa sasa wa golikipa huyo mwenye umri wa miaka 28 unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2019/20, baada ya kuongezewa mwaka mmoja na klabu hiyo na kumfanya De Gea abakie hapo Old Trafford.

Hata hivyo, sasa klabu hiyo inahofia wawakilishi wa golikipa huyo wanataka kuongeza kiasi kikubwa zaidi, kwa mujibu wa ESPN.


Manchester United imeripotiwa imempa ofa De Gea ya miaka mitano na mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki, ambapo utamfanya kuwa mchezaji wa tatu anayelipwa zaidi nyuma ya Paul Pogba na Alexis Sanchez, lakini sasa klabu hiyo inahofia huenda wasifikie makubaliano.

Kama Man United itakubali kumsainisha mkataba wa miaka mitano wa pauni milioni 90, utamfanya De Gea kuwa golikipa anayelipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha wa wakati wote.

Zote Paris Saint-Germain na Juventus zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili De Gea katika miaka ya hivi karibuni na hivyo kuonekana kwamba majaliwa yake ya kukaa hapo Old Trafford kuwa shakani.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LIVER ITAIULIA BAYERN KWAO - HENDERSON

Lakini tunao uzoefu kwenye Ligi ya Mabingwa na ninahisi kama tunaweza kwenda pale na...

**LIVERPOOL, England**

NAHODHA na kiungo wa kati wa Liverpool, Jordan Henderson, anaamini wanaweza kuisababishia matatizo Bayern Munich kwao wakati wa mechi ya marudiano ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vinara hao wa Ligi Kuu England juzi walilazimishwa sare tasa katika mechi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Anfield wakati timu zote zikihaha kusaka nafasi ya kutupia.

Lakini Henderson anaona Liverpool inaweza kufanya kitu fulani cha kuiangamiza Bayern ikiwa katika Uwanja wake wa Allianz Arena hapo Machi 13, mwaka huu.

"Kwenda ugenini pale, tunajua ni kwa namna gani walivyo wazuri kama timu, tunajua itakuwa vigumu," nahodha huyo aliiambia BT Sport.

"Lakini tunao uzoefu kwenye Ligi ya Mabingwa na ninahisi kama tunaweza kwenda pale na kuwajeruhi."

Sadio Mane na Mohamed Salah walipata nafasi nzuri kwa Liverpool, lakini walishindwa kuzitumia katika mechi hiyo.

Hata hivyo, Henderson anaamini kikosi chao kilifanya vyakutosha kusaka nafasi ya kusonga mbele, lakini akakiri wawili hao walishindwa kumalizia shughuli katika nafasi walizozipata.

"Ni wazi inakatisha tamaa hatukuweza kufunga. Tulikuwa na nafasi za kutosha, ninahisi ya kufunga moja au mawili," alisema.

"Nadhani kiwango kilikuwa kizuri, tulikosa umakini katika umaliziaji. [nafasi] bado ipo wazi kwa uhakika.

"Tunazo mechi kabla ya [marudiano ugenini Munich] lakini bado tunahitaji kujiamini."

## KWA UFUPI

### GUARDIOLA AMTAKA RICE, BEN
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anamfuatilia kiungo wa West Ham, Declan Rice, 20, beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, na beki wa kushoto wa Leicester, Ben Chilwell, 22, wakati akitazama majira ya kiangazi kununua makinda wa Kiingereza wenye vipaji. ***(Sun)***

### ZIDANE, LAMPARD KAZI CHELSEA
Chelsea imebainisha kiungo wake wa zamani na kocha wa wa sasa wa Derby, Frank Lampard pamoja na aliyekuwa kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane kuwa ndio wanaoweza kurithi mikoba ya Sarri. ***(Sky Sports)***

### SANCHO AGEUKIWA UNITED
Manchester United imebainisha winga wa Borussia Dortmund, Jaden Sancho, 18, kuwa katika mawindo yao kuelekea usajili wa majira ya kiangazi, lakini inahisi itahitaji kwanza kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao ili kuweza kumshawishi nyota huyo wa kimataifa wa England kurudi EPL. ***(Mirror)***

### LAPORTE KUFUNGWA UPYA CITY
Manchester City inajiandaa kumpa ofa ya mkataba mpya beki Mfaransa Aymeric Laporte, 24, kufuatia kiwango chake kizuri msimu huu. ***(Times)***

### SARRI ANUKIA KUTIMULIWA J'PILI
KOCHA Mkuu wa Chelsea, Maurizio Sarri, atatimuliwa endapo atapoteza mechi ya Jumapili ya Kombe la Ligi [Carabao Cup] dhidi ya Manchester City. ***(Mirror)***

### BAYERN, CITY KWA BISSAKA
MIAMBA ya Ujerumani, Bayern Munich imejiunga katika orodha ya klabu zinazomfuatilia beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, ambaye pia anawindwa na Manchester City. ***(Mail)***

### DE GEA BADO MTIHANI UNITED
Manchester United bado inatumai kufikia makubaliano ya mkataba mpya na kipa wake, Mhispania David de Gea, 28, lakini kuna madai wakala wake anapandisha dau. ***(ESPN)***

### WENGER ATETA NA PSG
KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, amekutana na Rais wa Paris St-Germain, Nasser al-Khelaifi, katika michuano ya Tenisi ya WTA huko Doha wiki iliyopita, huku kukiwa na tetesi kuwa mabingwa hao wa Ufaransa hawana furaha na Mkurugenzi wao wa Michezo, Antero Henrique. ***(L'Equipe)***

### POPE ANUKIA KUMRITHI CECH
Arsenal inafuatilia maendeleo ya kipa wa Burnley, Nick Pope, 26, wakati wakiendelea kuchunguza mbadala wa Petr Cech, 26, ambaye atastaafu mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

### DI MARIA AANIKA YA VAN GAAL
STRAIKA Angel di Maria, amesema uhusiano wake na kocha wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal, ulipungua baada ya kuhoji staili ngumu ya uongozi wa Mholanzi huyo hapo Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### BARCA KWA PEPE, LEO
Barcelona imetuma timu yake ya mashushu kwenda kumtazama mshambuliaji wa Lille, Muivory Coast Nicolas Pepe, 23, na straika Mreno Rafael Leao, 19. ***(France Football)***

### SPURS NAYO YAMFUATA ADAMS
Tottenham imejiunga katika orodha kubwa ya klabu zinazomfuatilia straika wa Birmingham City, Che Adams, 22. ***(Birmingham Mail)***

### MILITAO BADO KIDOGO REAL
Real Madrid inakaribia kukamilisha dili la kumsajili beki Mbrazil Eder Militao, 21, kutoka Porto ya Ureno. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# CHIPUKIZI, ZIMAMOTO ZABEBA MOJA MOJA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Chipukizi kutoka Pemba imelazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Zimamoto katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi jioni kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Kutokana na matokeo hayo, Chipukizi ambayo imecheza michezo 20 hadi sasa, imefikisha pointi 19 na kuwa katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Chipukizi, Amirali Khamis alisema mechi hiyo ilikuwa na ushindani na anashukuru kupata pointi hiyo moja ambayo imemsaidia katika kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

Khamis alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana katika kila mechi watakayocheza ili wapate matokeo mazuri na hatimaye washishuke daraja.

"Timu yangu ilicheza vizuri na tulistahili kushinda, ila kupata matokeo ya sare kumetokana na mapungufu yaliyopo kwa washambuliaji ambao walishindwa kumalizia vizuri," alisema Khamis. Kocha huyo aliongeza kuwa amejipanga kuyafanyia kazi mapungufu yaliyopo katika kikosi hicho ili waweze kuzoa pointi katika mzunguko huu wa lala salama ikiwamo kutoruhusu kufungwa.

"Tutapambana kuhakikisha tunabakia katika Ligi Kuu Zanzibar, japo niseme ukweli msimu huu kuna ushindani hususan kwa timu ambazo zipo mkiani katika msimamo wa ligi," aliongeza kocha huyo.

Hata hivyo, kocha huyo amewaomba waamuzi wanaochezesha ligi hiyo kuzingatia kanuni za mchezo huo ili kuondoa malalamiko ya mara kwa mara na mvutano kati ya viongozi wa klabu na maofisa hao.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 19 ndiyo inatoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo hufanyika kila mwaka kwa usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

**KAZI KWELI...**



Lionel Messi (chini mbele), katika harakati za kuipa ushindi Barcelona wakati wakilazimisha sare tasa dhidi ya Lyon, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-Bora katika Uwanja wa Groupama, Ufaransa juzi. **PICHA: MTANDAO**

# TFF wamlilia Kamishna Mchau

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Kamishna wa Ligi Kuu na aliyekuwa mwamuzi wa kimataifa mstaafu, Charles Mchau kilichotokea jana katika Hospitali ya KCMC iliyoko Moshi, Kilimanjaro.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, ilisema kifo cha Mchau ni pengo katika tasnia ya soka kutokana na mchango wake aliokuwa anautoa kwenye kuendeleza mchezo huo.

Ndimbo alisema shirikisho hilo linawapa pole familia pamoja na wadau wote kutokana na msiba huo. "Nimepokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha Mchau ambaye alikuwa bado anautumikia mpira wa miguu, kwa niaba ya TFF natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wao, Mungu awape subira katika kipindi hiki kigumu na cha majonzi," alisema Rais wa TFF, Wallace Karia.

Ibrahim Kidiwa wa jijini Tanga ambaye pia ni Kamshna wa Ligi Kuu alisema ameumia sana kwa kuondokewa na mdau huyo ambaye walikuwa wakichezesha wote mpira enzi zao.

"Tulikuwa naye katika mechi ya Coastal na Yanga Mkwakwani, alisema alikuwa anasumbuliwa na vidonda vya tumbo, nimeshtuka sana," alisema Kidiwa.

# ZFA yawafungia 'mabondia' New Boys

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WACHEZAJI watatu wa New Boys inayoshiriki Ligi Daraja la Pili wamefungiwa kucheza soka kwa muda wa miaka miwili kutokana na kubainika na kosa la kuwapiga waamuzi waliochezesha mechi ya Kombe la FA, imefahamika.

Nyota hao waliwapiga waamuzi wakati timu yao ilipokuwa inacheza dhidi ya Kilimani City kwenye Uwanja wa Wimbi, na timu yao kufungwa mabao 3-2.

Makamu Mwenyekiti waKamati ya Mashindano ya Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), Hus sein Ahmada aliwataja wachezaji hao walio fungiwa kuwa ni Mpango Abdallah, Ussi Mohmed na Zaharani Mcha.

Ahmada alisema wachezaji hao walitenda kosa hilo katika mchezo huo uliochezwa Februari 10, mwaka huu baada ya kudai kuwa bao la tatu lililofungwa na wapinzani wao lilikuwa la kuotea.

Alisema mbali na kuwafungia wachezaji hao, kamati hiyo pia imeipiga faini ya Sh. milioni mbili timu ya New Boys ili kulipia mali zilizoharibiwa pamoja na maandalizi ya mchezo huo ikiwamo gharama za matibabu ya waamuzi ambao waliumia.

Aliongeza kuwa faini hiyo inatakiwa kulipwa kabla ya mwezi huu haujamalizika na uamuzi uliotolewa uwe fundisho kwa timu nyingine kutojihusisha na vitendo vya kuvunja sheria na badala yake wanatakiwa kuwasilisha malalamiko yao kwa kufuata utaratibu.

"Hivi vitendo vya kuwapiga waamuzi vinazidi kushika kasi sana, sasa sisi kamati hatutalifumbia macho, iwapo timu inahisi imeonewa inatakiwa kufuata sheria zilizopo ikiwamo kuwasilisha malalamiko yao, lakini sio kujichukulia jukumu la kuwapiga waamuzi," alisema Ahmada.

Aliwataja waamuzi waliopigwa kuwa ni Mfaume Ali ambaye alikuwa anapuliza filimbi pamoja na wasaidizi wake, Dalila Jaffar, Khamis Juned na Ramadhani Nassor ambaye alikuwa Kamisaa wa mechi hiyo.

# Singida, Coastal kukipiga Chamazi

**Na Mwandishi Wetu**

MECHI ya Kombe la FA kati ya Singida United na Coastal Union iliyopangwa kuchezwa keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Namfua, sasa itapigwa Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Mkurugenzi wa Singida United, Festo Sanga, aliliambia gazeti hili jana kuwa wanaishukuru Bodi ya Ligi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kukubali ombi lao la kubadilisha uwanja utakaochezewa mchezo huo.

Sanga alisema uamuzi wa kuomba mabadiliko ya uwanja ulitokana na changamoto ya ratiba waliyonayo ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano hiyo ya Kombe la FA ambayo itaendelea mwishoni mwa wiki hii.

"Kutokana na ugumu wa ratiba yetu ya Ligi Kuu na Kombe la FA, mchezo wetu dhidi ya Coastal Union wa Kombe la FA sasa utachezwa Dar es Salaaam Februari 23, mwaka huu badala ya Namfua kama ulivyopangwa awali, ikumbukwe leo Jumatano (jana) Singida United inacheza dhidi ya Ndanda FC mjini Mtwara,...halafu timu inatakiwa iondoke Mtwara kurejea Singida kwa umbali wa Mtwara hadi Singida ni safari ya siku mbili, hivyo timu ingefika Singida Februari 22 (kesho)," ilisema sehemu ya taarifa ya Sanga.

Aliongeza kuwa, pia Singida United ililazimika kupeleka maombi hayo kwa ajili ya kuthamini afya za wachezaji na umuhimu wa mchezo husika.

Alisema wanaishukuru TFF kwa kukubali ombi lao na vile vile wanawaomba radhi mashabiki na wakazi wa Singida kwa uamuzi huo waliouchukua.

Michezo
Alhamisi Februari 21, 2019
Nipashe



## Liver itaiulia Bayern kwao - Henderson

HABARI UK 30

# YANGA SC YAANGUSHA MNINGA WA KIRUMBA

●●●Ni baada ya misimu miwili hatimaye Mbao FC imekubali kichapo kwa mara ya kwanza huku...

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

YANGA ni kama imefanikiwa kuangusha mti imara wa mninga uliowashinda katika Uwanja wa CCM Kirumba tangu msimu wa 2016/17 na kuuchana mbao, hiyo ikiwa ni baada ya jana kufanikiwa kuichapa Mbao FC kwa mabao 2-1 kwa mara ya kwanza katika dimba hilo la jijini Mwanza.

Tangu Mbao FC ilipopandishwa Ligi Kuu na Shirikisho la Soka nchini (TFF) msimu wa 2016/17, baada ya Kamati ya Nidhamu kufuta matokeo na kuzishusha daraja timu nne za Geita Gold Mine, Polisi Tabora, JKT Oljoro na JKT Kanembwa kufuatia kubainika kuwa zilipanga matokeo kwenye mechi za Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, Yanga haijawahi kuifunga timu hiyo katika Uwanja wa CCM Kirumba.

Mbao imekuwa ikiichapa Yanga katika uwanja huo, huku Wanajangwani hao nao wakishinda wakiwa dimba lao la nyumbani jijini Dar es Salaam.

Msimu wa kwanza Mbao iliichapa Yanga bao 1-0 lililofungwa na Habib Kyombo Mei 20, 2017 na uliofuata msimu wa 2017/18, ikashinda 2-0, yote yakifungwa tena na Kyombo, hiyo ikiwa ni Desemba 31, 2017.

Hata hivyo, Mbao FC imekuwa nyanya kwa Yanga inapocheza jijini Dar es Salaam. Kwenye mechi tatu zilizocheza imefungwa zote. Mechi ya kwanza tangu ipande Ligi Kuu ilikuwa ni Oktoba 30, 2016 kwenye Uwanja wa Uhuru ilipofungwa mabao 3-0, kabla ya kufungwa bao 1-0 msimu uliofuata Mei 22, mwaka jana.

**Msimu huu kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, Yanga iliichapa Mbao mabao 2-0, Oktoba 7, mwaka jana katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Katika mechi ya jana, bao la pili lililofungwa kwa njia ya penalti na Amissi Tambwe lilitosha kuipa Yanga ushindi huo wa mabao 2-1 na kujiimarisha kileleni mwa ligi hiyo kwa kufikisha pointi 61 baada ya kucheza mechi 25 wakati Mbao FC wanaofundishwa na Ali Bushiri hiyo ikiwa ni mechi yao ya 27 wakiwa na alama 36.

Mwamuzi Ally Simba alitoa penalti hiyo baada ya beki wa Mbao FC kuunawa mpira katika eneo la hatari akijaribu kuokoa krosi iliyopigwa na beki wa kati wa Yanga, Kelvin Yondani katika dakika ya 68.

Awali alikuwa ni mshambuliaji wa Mbao FC, Ndaki Robert ambaye alianza kuifungia kwa kichwa timu yake baada ya kuunganisha krosi safi iliyopigwa kwa mguu wa kushoto na Amos Charles na kuwafanya wenyeji wa mchezo huo kwenda mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0.


Mbao FC ndio waliofanya mashambulizi zaidi katika kipindi hicho cha kwanza ukilinganisha na wapinzani wao Yanga, lakini washambuliaji wake walipoteza nafasi walizozitengeneza katika mchezo huo.

Dakika ya 21 Mbao FC walipoteza nafasi ya kufunga baada ya Amos kupiga shuti nje na kupoteza krosi iliyotengenezwa na Said Said Jr na dakika iliyofuata Yanga ilijibu shambulizi hilo kupitia kwa Amissi Tambwe aliyepokea krosi kutoka kwa Ibrahim Ajibu, lakini mpira wa kichwa aliopiga ulikwenda nje.

Wakati huo huo jijini Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Uhuru, wenyeji KMC walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar wakati Stand United ikiwa nyumbani Shinyanga ilikubali kulazimishwa sare ya mabao 2-2 na Lipuli FC kutoka Iringa huku Ndanda FC ikiwafunga Singida United mabao 2-0.

Salum Kimenya alifanikiwa kuipa ushindi Tanzania Prisons baada ya kufunga bao pekee katika mechi ya 'Mbeya Derby" iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini humo.

OKOA...



Kipa wa Liverpool, Alisson, akiokoa hatari wakati wa mechi ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich, iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Anfield na kumalizika kwa sare tasa. **HABARI UK. 28**

# Simba: 'Kituo kinachofuata ni Bakhresa'

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kimerejea jijini Dar es Salaam huku Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems, akisema kazi inayofuata sasa ni dhidi ya Azam FC na kwamba watajiimarisha kwa lengo la kuhakikisha wanaendelea kuwapa furaha ya ushindi mashabiki wa timu hiyo.

Simba ilirejea jijini ikitokea Arusha na kesho Ijumaa itakutana na timu hiyo inayomilikiwa na bilionea Said Salim Bakhresa, Azam FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Taifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems alisema aliamua kupumzisha baadhi ya nyota wake wanaocheza kikosi cha kwanza kwa ajili ya kuwasubiri Azam FC ambao nao pia walikuwa na mechi ya ugenini jijini Tanga dhidi ya Coastal waliyolazimishwa sare ya bao 1-1. Aussems alisema anaamini wachezaji wake wataendelea kujituma na kucheza kwa bidii ili wapate pointi nyingine tatu katika mechi hiyo na baadaye watakapoifuata Lipuli FC mkoani Iringa.

Alisema licha ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya African Lyon juzi, mchezo huo ulikuwa mgumu kutokana na changamoto ya uwanja ambao iliwalazimisha wabadilishe mfumo wa kucheza.

"Azam ilicheza jana (juzi), na sisi pia tulicheza jana (juzi), tuna wachezaji wengi na kila mmoja atapata nafasi ya kucheza kutokana na mahitaji tuliyokuwa nayo, uwanja haukuwa mzuri na hii ilitufanya tusicheze mfumo wetu uliozoeleka, kikubwa ilikuwa ni pointi tatu na tunashukuru tulizipata, naamini tutaendelea kuwapa furaha mashabiki wa Simba," alisema Aussems.

Aliongeza kuwa timu yake pia ilikuwa na uchovu kwa sababu ilitoka kwenye mechi kubwa mbili dhidi ya (Al Ahly kisha Yanga), hivyo alilazimika kuwapumzisha baadhi ya wachezaji wake kwa faida ya mchezo unaofuata.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa beki wake Erasto Nyoni anatarajiwa kujiunga na mazoezi ya pamoja Jumatatu na mambo yakienda vema huenda akawa kwenye kikosi kitakachosafiri kuelekea Algeria kuwavaa JS Saoura katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >